SportPesa
TZS. 559,183,880
BET LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Mvutano** kati ya DC na m'kiti aliyemsimamisha wachukua sura mpya

UKURASA 7




**Conte: Chelsea haijui kumtumia Lukaku**

UKURASA 23


# Nipashe

Jumanne Oktoba 5, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580724

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# Mawaziri 8 waenda vijiji kutatua migogoro ardhi

• **Ni** agizo la Rais Samia mikoa 10 kwenye vijiji 920...*Uk.2*



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza alipofungua Kongamano la Tano la Uwezeshaji Mwananchi Kiuchumi kwenye Ukumbi wa PSSSF Makole jijini Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

## YALIYOMO


UKURASA WA 2

**MAJALIWA: CHANJO UVIKO YAFIKIA 80%**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema kuwa tangu kuanza kwa zoezi la uchanjaji chanjo ya UVIKO-19 nchini...

UKURASA WA 3

**SAMIA, KIGOGO ROYAL DUTCH SHELL WATETA**

RAIS Samia Suluhu Hassan, jana amezungumza kwa njia ya mtandao na Ofisa Mtendaji Mkuu wa...

UKURASA WA 4

**TANESCO YAOMBA RADHI TATIZO LA LUKU**

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO), limewaomba radhi wateja wake kwa tukio lililotokea jana la...


## Lori lapata ajali Dar, wananchi waiba saruji

UKURASA 3




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (wapili kushoto), akimkabidhi hati ya kiapo cha huduma kwa wateja Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka (watatu kushoto), baada ya uzinduzi rasmi wa hati hiyo uliofanyika jijini Dodoma jana, ikiwa ni maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja. Wengine ni Mbunge wa Jimbo la Dodoma Mjini, Anthon Mavunde (kushoto), Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara, Filbert Mponzi (kulia), Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Mukunda (wapili kulia), na Mbunge wa Jimbo la Bahi, Keneth Nolo. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Jiko la mkaa lilivyoua familia usiku

UKURASA 2

**MICHEZO** **KIBU FASTA AJIUNGA TAIFA STARS** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Mawaziri 8 waenda vijijini kutatua migogoro ya ardhi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TIMU ya mawaziri wanane iliyopewa maagizo maalum na Rais Samia Suluhu Hassan Suluhu ya kuzunguka kwenye maeneo ya migogoro kati ya wananchi na hifadhi kwenye vijiji 920 nchini, imeanza kazi hiyo leo ili kufanya uhakiki wa kina na kumaliza tatizo hilo.

Timu hiyo inahusisha Waziri wa Nchi TAMISEMI, Maliasili na Utalii, Maji, Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Ulinzi, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira na Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambapo itaanza kwa kutembelea mikoa 10.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alitaja mikoa hiyo ni Dodoma, Singida, Manyara, Tabora, Mbeya, Morogoro, Dar es Salaam, Pwani, Mara na Geita na baadaye watamalizia kwenye mikoa iliyobaki.

Alieleza kuwa kazi hiyo itaanza leo (jana) hadi Oktoba 20, mwaka huu ili kutekeleza agizo la Rais Samia na kutoa matokeo juu ya vijiji vilivyopata msamaha na kuamriwa wananchi wabaki kwenye maeneo hayo yaliyohifadhiwa kwa ajili ya shughuli mbalimbali za mifugo na kilimo.

"Kesho (leo) tunaanza Mkoa wa Dodoma Wilaya ya Chemba na Kondoa eneo la Mkungunero na maeneo mapya ambayo misitu itapunguzwa," alisema.

Alifafanua kuwa katika vijiji 920 walivyokwenda walibaini vimevamiwa na wananchi na serikali ikaamua visiondolewe kwa wananchi licha ya kuwa vipo vichache ambavyo vitaondolewa kwa wananchi kutokana na tathmini kuonyesha ni hatarishi kwa usalama wao.

"Ilionekana ni hatarishi pia kwa viumbe na raia kwa mfano kwenye vyanzo vya maji kama Bwawa la Nyerere, tutatoa taarifa kwa mikoa yote nchini hususani vijiji hivyo vilivyotolewa uamuzi na Rais hasa vilivyopo kwenye maeneo ya mbuga, na hii ni fursa kwa viongozi wa Mkoa kutoa taarifa kama kuna mgogoro mkubwa zaidi kwenye eneo lako, tunaenda kumaliza migogoro inayotokana na vijiji 920 ambavyo havitaondoka kwenye maeneo hayo ndani ya mwaka huu," alisema.

Lukuvi alisema tathmini itafanyika kwenye maeneo hatarishi kwanza yaliyopo kwenye Mikoa ya Morogoro na Mbeya ambayo Rais ameagiza yaachwe kwa shughuli za kilimo na mifugo.

Alisema baada ya uamuzi wa Rais wataenda kufanya tathmini ni maeneo gani yabaki na yapi yatolewe licha ya kuwa mengi yatabaki hivyo.

"Viongozi wazuie uvamizi kufanyika kwenye maeneo ya hifadhi maana zoezi hili halitakuwa likifanyika mara kwa mara hivyo wananchi watii sheria," alisema.




Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya CRDB, Dk. Ally Laay (watatu kulia) na Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Heri James, wakikata utepe kuashiria uzinduzi wa Wiki ya Huduma kwa Wateja katika hafla iliyofanyika tawi la Benki ya CRDB Mlimani City Dar es Salaam. Wengine kutoka kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Prof. Neema Mori, Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi, Mirand Naiman na Mkuu wa Kitengo cha Huduma kwa Wateja, Yolanda Uriyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jiko la mkaa lilivyoua familia usiku

**Na Richard Makore,** MWANZA

MOTO uliotokana na jiko la mkaa umesababisha vifo vya watu watatu akiwamo mama na watoto wawili katika Kijiji cha Busanda Kata ya Busanda wilayani Geita mkoani Geita.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu jana Kamanda wa Polisi mkoani Geita, Henry Mwaibambe, alikiri kutokea kwa vifo hivyo usiku wa kuamkia jana.

Kamanda Mwaibambe alimtaja mama huyo kuwa ni Unice Kulwa (25) na wanawe wawili walipoteza maisha baada ya kukosa hewa kutokana na kuingiza ndani jiko la mkaa walilokuwa wakipikia maharage kwenye nyumba waliyokuwa wamelala.

Aidha, alisema kwamba baba wa familia hiyo, Kurwa Kamili, alinusurika kifo na kwa sasa amelazwa Kituo cha Afya Katoro kwa ajili ya kupatiwa matibabu.

"Ndugu mwandishi ni kweli tukio hilo limetokea huko Busanda na waandishi wenzako wamenipigia simu, ninachoweza kusema ni hicho na sasa nipo 'busy' na maandalizi ya Mwenge," alisema Kamanda Mwaibambe.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Geita, Wilson Shimo, naye alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema limetokea usiku wa kuamkia Oktoba 3, 2021 katika Kitongoji cha Shilungule, Kijiji cha Busanda wilayani humo.

Katika tukio hilo, watoto waliopoteza maisha ni Kamuli Kulwa (5) na Jenipha Kulwa (3).

Imeelezwa kuwa mama huyo baada ya kumaliza kupika chakula cha usiku alibandika maharage kwenye jiko la mkaa na kisha kukiingiza ndani na kufunga mlango na kulala.

Kutokana na hali hiyo, ilielezwa kwamba majirani walihisi hali ya tofauti na walipotoka nje walibaini kuna shida ndani ya nyumba hiyo.

Baada ya majirani hao kuhisi hali hiyo waliamua kuamshana na kisha wakakubaliana kugonga mlango kwa marehemu.

Majirani hao baada ya kugonga mlango bila mafanikio waliamua kuuvunja na kisha kuingia ndani na kukuta wanafamilia hao wakiwa hawajitambui na kuwakimbiza hospitali.

Hata hivyo, mama na watoto hao walifariki, huku baba akiwa bado anaendelea kupata matibabu.

# Majaliwa: Chanjo UVIKO yafikia 80%

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema kuwa tangu kuanza kwa zoezi la uchanjaji chanjo ya UVIKO-19 nchini hadi sasa limefikia zaidi ya asilimia 80 na kiasi kidogo cha chanjo kimebakia mikoani.

Majaliwa, alibainisha hayo jana jijini hapa wakati alipokuwa akifungua kongamano la tano la kitaifa la uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Alisema suala la kuchanja ni muhimu kwa kila mtu kwa kuwa inasaidia kupunguza madhara kwa mgonjwa wa corona tofauti na asiyechanjwa.

"Tulisema chanjo hii ni hiari, lakini ni muhimu sana kila Mtanzania akachanjwa kwa sababu inaleta virutubisho ndani ya mwili kupambana na magonjwa yanapoingia pia ukipata ugonjwa huwezi kuwa 'serious' sana kama mtu ambaye hajachanja kabisa.

"Tumeona katika mataifa ya wenzetu wapo katika hali nzuri siku hizi wameacha hata barakoa wanafanya shughuli zao kwa sababu kila mmoja amechanja na wote wanauhakika na afya zao nasiye tungependa tufikie hapo," alisema Majaliwa. Alisema watu wajitokeze kwa wingi kuchanja, ili kuwa na uhakika na kinga ndani ya nchi.

"Tuliagiza eneo kama hili ambapo kuna mkusanyiko mkubwa lazima kuwapo na huduma ya utoaji wa chanjo hii kwani watu wengi tunakuwa bize sana na kazi, lakini hapa unaweza kwenda kuchanja na kurudi kuendelea kujadiliana na wenzako kwani chanjo hii haimzuii mtu kuendelea na kazi zake," alisisitiza Majaliwa.

Alisema kila mtu anatakiwa kutambua umuhimu wa afya yake na kuacha kusikiliza maneno ya watu wengine, ambao wamekuwa wakipotosha zoezi hilo.

"Hali inaonekana kama kutulia hivi, lakini tatizo hili bado lipo tuendelea na kujikinga kwa kuchukua tahadhari zote sio kujilinda hapa tu tulipo na baada ya kuondoka hapa tunapuuza," alisisitiza.

Vilevile, aliwataka wakuu wa mikoa nchini kuendelea na utoaji wa elimu pamoja na kuwafikia wananchi katika maeneo yao, ili kuwapatia chanjo.

"Ndugu wakuu wa mikoa endeleeni na elimu na hamasa kwa wananchi na wafikieni niliona mtu mmoja ofisa wetu wa afya kule Tunduru amebeba begi lake na chanjo anapita kurahisisha upatikanaji wa chanjo," alisema.

Akizungumzia kongamano hilo alisema serikali imedhamiria kutekeleza dhana ya uchumi jumuishi kwa vitendo kwa kuweka vipaumbele vitakavyowawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi.

Alisema, vipaumbele katika mipango ya serikali vimekuwa katika utekelezaji wa shughuli za kiuchumi zinazowajumuisha moja kwa moja wananchi.

Waziri Mkuu alitaja baadhi ya vipaumbele hivyo kuwa ni pamoja na uimarishaji wa huduma za afya, hifadhi ya jamii, maji, umeme na utekelezaji wa mpango wa elimu msingi bila ada.

"Mtanzania mwenye afya, aliyeelimika na miundombinu wezeshi ni chachu kwa ukuaji uchumi wa nchi yetu," alisema. Pia, alisema serikali imeandaa sera mbalimbali, ambazo zimelenga kuhakikisha kunakuwa na maendeleo endelevu na uchumi jumuishi.

Kadhalika, Waziri Mkuu ametoa maagizo kwa viongozi wa wizara, mikoa, taasisi za umma na binafsi pamoja na wadau wa masuala ya uwezeshaji kuhakikisha dhamira ya dhati ya Rais Samia ya kuiwezesha nchi kuwa na uchumi jumuishi inatimia.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Geoffrey Mwambe, aliwaagiza wakuu wa mikoa wahasimamie ipasavyo shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi katika maeneo yao, ili kuwa na tija katika kuhakikisha malengo ya Rais Samia yanafikiwa.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Beng'i Issa alisema baraza hilo limeendelea kuratibu na kusimamia mifuko ya uwezeshaji wananchi kiuchumi, ambayo kwa kushirikiana na ile inayotoa dhamana imefanikiwa kutoa mikopo yenye thamani ya Sh. trilioni 4.97 kwa wajasiriamali 7,231,617.

Alisema baraza hilo limesimamia uanzishwaji wa vituo vya uwezeshaji wananchi kiuchumi katika mikoa mbalimbali ambapo kwa sasa vimefikia 17 katika mikoa sita ya Geita, Shinyanga, Singida, Rukwa, Dodoma na Kigoma, ambavyo katika kipindi cha mwaka mmoja vimefanikiwa kutoa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 24 kwa wafanyabiashara 3,233 na mafunzo ya ujuzi na biashara kwa watu 1,990.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, akimkabidhi nyaraka mmoja wa wajumbe wa Bodi ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) Abdulaziz Alladin Shambe. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Rais Samia azungumza na kigogo Royal Dutch Shell

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, jana amezungumza kwa njia ya mtandao na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Royal Dutch Shell, Ben Van Beurden, yenye makao yake makuu nchini Uholanzi.

Taarifa iliyotolewa na Ikulu, ilisema Beurden amemshukuru Rais Samia na kueleza kuwa wanaridhishwa na jinsi Serikali ya Awamu ya Sita ilivyoboresha mazungumzo ya uwekezaji kwenye mradi wa gesi asili, iliyosindikwa (LNG) hapa nchini.

Kwa upande wake Rais Samia amemshukuru Beurden kwa nia yao ya kutaka kuwekeza kwenye mradi huo, ambao utachochea kukuza uchumi wa Tanzania.

Kikao hicho kilichofanyika kwa njia ya mtandao Ikulu Chamwino mkoani Dodoma, kimehudhuriwa na Waziri wa Nishati, January Makamba, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk, Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Dk. James Mataragio.

# Lori lapata ajali Dar, wananchi waiba saruji

**Na Elizabeth Zaya**

WAKAZI wa Mbagala, Wilaya ya Temeke, jijini Dar es Salaam jana walivamia lori la saruji na kuanza kuiba baada ya kupata ajali katika eneo la Misheni, Mtaa wa Kizinga katika kata hiyo ya Mbagala.

Kwa mujibu wa mashuhuda waliokuwa eneo hilo, baada ya lori hilo kufika eneo la Misheni lilifeli breki na kuanza kuteremka chini kwenye makazi ya watu na kugusa daladala mbili kwa upande wa nyuma pamoja na nyumba.

Ramadhani Hassan ni miongoni wa mashuhuda waliokuwapo eneo la tukio ambaye alisema, baada ya kutokea ajali hiyo, wananchi hao walivamia na kuanza kuchukua mali za watu waliokuwamo katika lori hilo, pamoja na kuanza kuiba saruji hiyo.

Alisema baada ya watu hao waliokuwamo kwenye lori kuona hivo, walikimbia kujiokoa na kuacha vitu vyao.

"Baada ya lori kufeli breki, liligusa kidogo daladala mbili kwa nyumba likateremka huko chini na baada ya hapo ndipo watu wakaanza kuvamia na kuchukua saruji, tumeshuhudia wanawake kwa wanaume wote kwa ujumla wao wakibeba sementi kwa wingi, lakini tunashukuru baada ya askari kufika wakawatawanya wakakimbia,"alisema Hassan.

"Waliokuwamo kwenye lori walikuwa wanne wamekaa mbele kule, lakini lilivyofeli, watu wakavamia mabegi yao na kuanza kuwasachi, ikabidi wakimbie na kondakta akaenda kujificha nyuma ya hospitali na tumeona mmoja ndio ameumia mguu, ila wengine walitoka salama."

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Mulioo, alisema tukio hilo lilitokea saa nne asubuhi na kwamba lori hilo namba T.342 DJZ likiwa na tela lake namba T.154 DKC lilipofeli breki na kushindwa kukata kona katika eneo hilo la Misheni, Mbagala.

"Lilipofika Mbagala eneo la Misheni kwenye mteremko mkali likashindwa kukata kona na kutumbukia chini, tairi zilipasuka na watu wakaanza kuiba saruji,"alisema Kamanda Muliro.

"Askari walifika mapema na kuokoa mifuko ya saruji 375, ambayo ilienda kuchukuliwa na gari jingine la kampuni moja, mifuko 82 mingine ya saruji hiyo ilipasuka."

Kamanda Muliro alisema lori hilo halikugonga daladala wala nyumba na kwamba dereva alikimbia kutokana na taharuki ya wananchi ya waliovamia.




# CEGODETA yataka wadau wengi kwenye sensa 2022

**Na Sabato Kasika**

SERIKALI imeshauriwa kushirikisha wadau wengi katika utoaji wa elimu kuhusu sensa ya watu na makazi, wasaidie Watanzania kutambua umuhimu wake, ili wakati wa kuhesabiwa utakapofika washiriki kikamilifu.

Wito huo ulitolewa jijini Dar es Salaam na Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), Thomas Ngawaiya, alipokuwa akizungumzia umuhimu wa sensa ya watu na makazi.

Alikuwa akielezea mtazamo wa taasisi hiyo na kufafanua kuwa baadhi ya watu wamekuwa hawahesabiwi kutokana na ukosefu wa elimu ya kutosha ya kutambua manufaa ya sensa.

"Ushauri wetu kwa serikali ni kwamba ishirikishe wadau wengi katika utoaji wa elimu kuanzia kwenye asasi za kiraia, vyama vya siasa na wengine, ili wasaidie Watanzania watambue umuhimu wa sensa," alisema Ngawaiya.

Alisema sensa ina umuhimu mkubwa, kwa kuwa ndiyo inayosaidia serikali kupata taarifa za msingi zitakazowezesha mchakato wa utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo ya Watanzania na taifa kwa ujumla.

"Bila kuwapo sensa, serikali haiwezi kujua idadi ya wananchi wake na inakuwa vigumu kupanga mikakati ya maendeleo, hivyo suala la elimu kwa Watanzania ni la muhimu, hasa likishiriklisha wadau wengi zaidi," alisema.

Ngawaiya alifafanua kuwa kuna suala la pato la mtu mmoja mmoja, pato la taifa, ajira na ukosefu wa ajira na kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi na kwamba hayo yote yanatakiwa kujulikana kwenye sensa.

"Nchi hii ni kubwa, hivyo kuna umuhimu wa kuwapo kwa watoa elimu wengi zaidi kuanzia wakati huu, ili kufikia Agosti mwaka ujao, iwe ni rahisi kila mtu kuhesabiwa, ili kusiadia serikali kupata takwimu sahihi za watu," alisema.

Aidha, alisema taasisi yake inaipongeza serikali kwa madodoso, ambayo imeandaa ili kufanikisha sensa yakianzia taasisi, ambazo ni mahsusi kwa wasafiri, watu watakaokuwa wamelala hotelini au nyumba za wageni na wagonjwa watakaokuwa wamelazwa hospitalini.

Alitaja dodoso lingine kuwa ni la wasio na makazi maalum, ambalo litakuwa mahsusi kwa watu wote wanaolala maeneo yasiyo rasmi, kwenye baraza za majengo mbalimbali, katika madaraja na maeneo mengine.

"Ukisoma madodoso yote, utagundua kuwa lile la dini ambalo limekuwa likilalamikiwa kwa muda mrefu halipo tena, sisi CEGODETA tunaona hilo la dini halina umuhimu, kwa sababu serikali haina dini," alisema.

Alifafanua kuwa katika sensa ya mwaka 2012, dodoso hilo lilitaka kusababisha baadhi ya watu wagome kuhesabiwa na kwamba taasisi hiyo, inaona hatua iliyochukuliwa na serikali ya kuondoa dodoso hilo ni nzuri.


Civil Procedure Code (Approved Forms)
G.N. No. 388 contd.

FORM NO. 4/1

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
JUDICIARY
IN THE DISTRICT COURT OF TANGA
AT TANGA
CIVIL CASE NO. 14 OF 2021
CONTRACTOR REGISTRATION BOARD PLAINTIFF(S)
VERSUS
RJ MUSSA CONSTRUCTION COMPANY LTD DEFENDANT(S)

SUMMONS TO FILE WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE
(O. V, r 1 CPC)

To: RJ MUSSA CONSTRUCTION COMPANY LTD

WHEREAS the above named Plaintiff(s) has/have instituted a suit against you upon the claim the particulars of which are set out in annexed copy of the plaint;

YOU ARE HEREBY NOTIFIED that you must file your WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE in duplicate within twenty one (21) days of service of this notice upon you. If there is more than one plaintiff, additional copies of your written statement of defence must be filed sufficient for service on each of the Plaintiffs. If there are more defendants than one and the defence is not joint defence, you must file sufficient copies for service on each of the other defendants.

AND TAKE NOTICE that if you default in filing the written statement of defence within the time specified, the court may pronounce judgment against you.

TAKE FURTHER NOTICE that the case also has been fixed for order before Honorouble R. E. NKISI - PRM Resident Magistrate on the 28 day of 10 2021 at 9:00 O'clock in the forenoon/afternoon

GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT 22 day of 09 2021

DISTRICT COURT TANGA

DISTRICT RESIDENT MAGISTRATE
P O Box 97
TANGA

Resident Magistrate

I HEREBY acknowledge the receipt of a duplicate of this summons this ........ day of ........ 20........

21648701


# TANESCO yaomba radhi tatizo la LUKU

**Na Christina Mwakangale**



SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO), limewaomba radhi wateja wake kwa tukio lililotokea jana la kutopatikana kwa huduma ya manunuzi ya umeme kupitia LUKU, hali iliyoleta usumbufu.

Limesema kukosekana kwa huduma hiyo kwa muda kulitokana na hitilafu ya mfumo wa manunuzi ya umeme.

Akizungumza na Nipashe kuhusu kadhia hiyo, Mkuu wa Uhusiano TANESCO, Johari Kachwamba (pichani), alisema hitilafu hiyo ilitokea asubuhi na kwamba hadi kufikia saa tisa alasiri huduma ilikuwa imerejea katika hali yake.

Kachwamba alisema tatizo hilo lilikuwa la kiufundi huku taarifa ya TANESCO ikiomba radhi kwa wateja wake kutokana na tatizo hilo.

Taarifa iliyotolewa na shirika hilo, ilieleza kuwa: "Tunawaomba radhi wateja wetu kutokana na hitilafu kwenye mfumo wa manunuzi ya umeme wa LUKU iliyotokea leo Oktoba 04, 2021 na kusababisha wateja kushindwa kununua umeme".

"Tayari wataalamu wetu wametambua tatizo na wanafanya kazi kuhakikisha linakwisha," ilisema taarifa hiyo jana.

Taarifa hiyo ilibainisha kwamba huduma ilirejea saa 9:00 alasiri, na kwamba wanaomba radhi kwa usumbufu uliojitokeza.

TANGAZO

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
## PRESIDENT'S OFFICE-REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
## MPANDA DISTRICT COUNCIL

# STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 30 JUNE 2020

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
MPANDA MUNICIPAL COUNCIL

### STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 30TH JUNE, 2020

| | Notes | 2020 TZS | 2019 TZS |
|---|---|---|---|
| **ASSETS** | | | |
| **Current assets** | | | |
| Cash and cash equivalents | 24 | 1,806,823,847 | 4,452,855,995 |
| Receivables and prepayments | 25 | 588,419,421 | 505,126,255 |
| Inventories | 26 | 65,882,393 | 261,293,582 |
| | | **2,461,125,660** | **5,219,275,832** |
| **Non-current assets** | | | |
| Other financial assets | 27 | 34,389,944 | 34,389,944 |
| Property, plant and equipment | 29 | 35,088,068,174 | 34,000,955,722 |
| | | **35,122,458,118** | **34,035,345,666** |
| **TOTAL ASSETS** | | **37,583,583,778** | **39,254,621,498** |
| **LIABILITIES** | | | |
| **Current liabilities** | | | |
| Payables | 35 | 831,866,864 | 726,922,157 |
| Employee benefits | 38 | 781,192,061 | 245,286,973 |
| Deferred income (Grant) | 11 | 149,079,920 | 381,287,985 |
| | | **1,762,138,844** | **1,353,497,115** |
| **Non-current liabilities** | | | |
| Provisions | 39 | 59,000,000 | 59,000,000 |
| Deferred Capital (Grant) | 41 | 1,122,676,653 | 3,994,351,518 |
| | | **1,181,676,653** | **4,053,351,518** |
| **TOTAL LIABILITIES** | | **2.943.815.497** | **5.406.848.632** |
| **NET ASSETS** | | **34,639,768,281** | **33,847,772,866** |
| **NET ASSETS** | | | |
| Accumulated surplus/(deficit) | | 34,605,378,337 | 33,847,772,866 |
| Minimum Compulsory Reserve | | 34,389,944 | - |
| **TOTAL NET ASSETS** | | **34,639,768,281** | **33,847,772,866** |

The financial statements were authorised for issue by the Council Management Team on 19th September, 2020 and were signed by:

Michael F. Nzyungu
**CMT Chairperson**
Date: 19/09/2020

Deodatus C. Kangu
**CMT Secretary**
Date: 19/09/2020

MUNICIPAL DIRECTOR
MPANDA MUNICIPAL COUNCIL
P.O. Box 216-MPANDA



THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
MPANDA MUNICIPAL COUNCIL

### STATEMENT OF FINANCIAL PERFORMANCE FOR THE YEAR ENDED 30TH JUNE, 2020

| | Notes | 2020 TZS | 2019 TZS |
|---|---|---|---|
| **Revenue** | | | |
| Taxes and levies | 9 | 1,420,298,129 | 1,125,022,771 |
| Fees, fines, penalties and licenses | 10 | 1,164,092,575 | 729,015,210 |
| Amortisation of revenue grants | 11 | 15,487,126,147 | 14,015,252,798 |
| Revenue from exchange transactions | 12 | 251,121,241 | 250,854,600 |
| Revenue from non-exchange transactions | 41 | 3,528,674,865 | 6,274,084,829 |
| Finance income | 13 | 1,549,000 | 2,046,575 |
| Other revenue | 14 | 485,102,649 | 615,164,360 |
| | | **22,337,964,606** | **23,011,441,142** |
| **Expenses** | | | |
| Wages, salaries and employee benefits | 18 | 15,026,306,954 | 13,046,362,280 |
| Supplies and consumables used | 19 | 2,170,181,822 | 2,351,593,239 |
| Maintenance expenses | 20 | 668,261,020 | 1,358,814,367 |
| Grants and other transfer payments | 21 | 234,351,930 | 1,376,529,163 |
| Provision for Impairment (Defaulters) | 25 | 156.122.063 | - |
| Provision for legal Case | 39 | - | 59,000,000 |
| Depreciation of property, plant and equipment | 29 | 1,271,146,599 | 594,988,367 |
| | | **19,526,370,388** | **18,787,287,416** |
| Share of associates surplus/(deficit) | | - | - |
| **Surplus/(deficit) during the year** | | **2,811,594,218** | **4,224,153,726** |
| | | - | - |

The financial statements were authorised for issue by the Council Management Team on 19th September, 2020 and were signed by:

Michael F. Nzyungu
**CMT Chairperson**
Date: 19/09/2020

Deodatus C. Kangu
**CMT Secretary**
Date: 19/09/2020

MUNICIPAL DIRECTOR
MPANDA MUNICIPAL COUNCIL
P.O. Box 216-MPANDA



THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
MPANDA MUNICIPAL COUNCIL

### CASH FLOW STATEMENT – DIRECT METHOD
### FOR THE YEAR ENDED 30TH JUNE, 2020

| | Note | 2019/20 TZS | 2018/19 TZS |
|---|---|---|---|
| **Cash flows from operating activities** | | | |
| **Receipts** | | | |
| Taxes and levies | 70A | 1,420,298,129 | 1,125,022,771 |
| Fees, fines, penalties and licenses | 70B | 1,019,630,512 | 729,015,210 |
| Recurrent Grants | 11 | 15,303,363,984 | 14,238,944,103 |
| Revenue from exchange transactions | 70C | 242,397,273 | 351,968,448 |
| Finance income | 13 | - | 2,046,575 |
| Other income | 70E | 485,102,649 | 631,637,528 |
| Change in Miscellaneous Deposit | 24 | 284,775,277 | 9,242,499 |
| **Total Receipt** | | **18,755,567,824** | **17,087,877,133** |
| **Payments** | | | |
| Employee costs | 70F | 14,490,401,866 | 12,908,538,663 |
| Payments to suppliers | 70G | 2,042,694,908 | 2,523,308,043 |
| Maintenance expenses | 70H | 668,296,102 | 1,343,178,703 |
| Grants and other transfer payments | 21 | 632,598,446 | 1,376,529,163 |
| Transfer of Fund to PMG | 11 | 48,445,902 | - |
| Other expenses | | - | 2,046,575 |
| **Total payments** | | **17,882,437,224** | **18,153,601,147** |
| **Net cash from operating activities** | | **873,130,600** | **(1,065,724,014)** |
| **Cash flows from investing activities** | | | |
| Acquisition of property, plant, and equipment & investment properties | 29 | (4,176,162,748) | (6,353,444,829) |
| **Net cash from investing activities** | | **(4,176,162,748)** | **(6,353,444,829)** |
| **Cash flows from financing activities** | | | |
| Development grants received | 41 | 657,000,000 | 4,934,880,464 |
| **Net cash used in financing activities** | | **657,000,000** | **4,934,880,464** |
| **Net increase in cash and cash equivalents** | | **(2,646,032,148)** | **(2,484,288,379)** |
| **Cash and cash equivalents at beginning of period** | 24 | **4,452,855,995** | **6,937,144,374** |
| **Cash and cash equivalents at end of period** | 24 | **1,806,823,847** | **4,452,855,995** |

The financial statements were authorised for issue by the Council Management Team on 19th September, 2020 and were signed by:

Michael F. Nzyungu
**CMT Chairperson**
Date: 19/09/2020

Deodatus C. Kangu
**CMT Secretary**
Date: 19/09/2020

MUNICIPAL DIRECTOR
MPANDA MUNICIPAL COUNCIL
P.O. Box 216-MPANDA



Mpanda Municipal Council,
P.O. Box 216,
MPANDA.

### 1.1 REPORT ON THE AUDIT OF FINANCIAL STATEMENTS

**Opinion**

I have audited the Financial Statements of Mpanda Municipal Council, which Comprise the Statement of Financial Position as at 30th June, 2020, and the Statement of Financial Performance, Statement of Changes in Net Assets and Cash Flow Statement and the Statement of Comparison of Budget and Actual Amounts for the year then ended, as well as the Notes to the Financial Statements, including a Summary of Significant Accounting Policies.

In my opinion, the accompanying Financial Statements present fairly in all material respects, the Financial Position of Mpanda Municipal Council as at 30th June, 2020, and its Financial Performance and its Cash Flows for the year then ended in accordance with International Public Sector Accounting Standards (IPSAS) Accrual basis of accounting and in the manner required by the Local Government Finances Act, 1982 (Revised 2000).

**Basis for Opinion**

I conducted my audit in accordance with International Standards of Supreme Audit Institutions (ISSAIs). My responsibilities under those standards are further described in the Auditor's Responsibilities for the Audit of the financial statements section of my report. I am independent of Mpanda Municipal Council in accordance with the International Ethics Standards Board for Accountants' Code of Ethics for Professional Accountants (IESBA Code) together with the National Board of Accountants and Auditors (NBAA) Code of Ethics, and I have fulfilled my other ethical responsibilities in accordance with these requirements.

I believe that the audit evidence I have obtained is sufficient and appropriate to provide a basis for my opinion.

Charles E. Kichere
**Controller and Auditor General**
**Dodoma, United Republic of Tanzania.**
**31st March, 2021**



216491702

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kutumia makanisa na misikiti elimu chanjo corona hatua muhimu

**UVIKO-19** ni miongoni mwa magonjwa ambayo yanaendelea kuangamiza maisha ya watu sehemu mbalimbali duniani. Hapa nchini, serikali imeamua kuandaa utaratibu wenye lengo la kuhakikisha inawakinga wananchi wake.

Kutokana na kuendelea kuwapo kwa ugonjwa huo, serikali imeanzisha utaratibu wa kutoa elimu inayohusu umuhimu wa kila Mtanzania kuchanja chanjo ya ugonjwa huo kwa waumini kanisani na misikini, baada ya ibada.

Hatua hiyo ya serikali tunaichukulia kama njia ambayo ni sahihi na itasaidia kuondoa dhana potofu iliyojengeka miongoni mwa jamii kuhusu chanjo hiyo kwamba ina madhara, hivyo kuwafanya watu wengi zaidi kuchanjwa.

Kitendo cha Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuzungumza na viongozi wa makanisa na misikiti mbalimbali nchini kwa lengo la kuanza kutoa elimu kwa waumini wao kila baada ya ibada na kutoa chanjo katika eneo husika, ni cha muhimu.

Tunaamini kwamba hiyo ni miongoni mwa njia ambazo zinaweza kusaidia Watanzania wengi kupata elimu sahihi kupitia kwa wataalamu wa afya pamoja na viongozi wao wa kiroho, ili kuongeza uelewa zaidi.

Ni matumaini yetu kwamba kupitia utaratibu huo Watanzania wengi watapata fursa ya kuelimishwa kisha kuona umuhimu wa kupokea chanjo ili wajikinge na maambukizi na kuwakinga wengine. Kwa mazingira hayo, tunadhani hata upotoshaji kuhusu chanjo ukakosa nafasi, hivyo kuwafanya Watanzania wengi kuendelea kujitokeza kupata huduma hiyo muhimu kwa ajili ya afya zao.

Lakini tunambua taasisi hizo ni wadau mkubwa wa sekta ya afya, kwa kuzingatia kuwa ziko katika mstari wa mbele kuwekeza kwenye afya kwa kujenga zahanati, vituo vya afya na hospitali ambazo zimekuwa zikitoa huduma kubwa za katika jamii.

Hatua ya taasisi hizo huduma za afya, ni wazi kwamba zinajali umuhimu wa waumini na Watanzania kwa ujumla kuwa na afya njema, hivyo tunaona kuwa hatua ya serikali ya kushirikisha viongozi wa dini katika vita hiyo ni sahihi.

Kwa kuwa taasisi hizo na viongozi wake ni wadau wakubwa wa masuala ya afya, tunaona kuna uwezekano kwa waumini kupata elimu inayokusudiwa kuwafikia, hasa wakati huu ambao nchi inapambana na ugonjwa huo.


Hivyo, wito wetu ni kwamba, waumini wawe tayari kupokea elimu hiyo kwa ajili ya kuwajengea uelewa utakaowasaidia kuepuka maambukizi, lakini kupata chanjo ili kuwa salama zaidi. Tunajua kuwa penye wengi pana mengi, inawezekana wakawapo baadhi ya watu watakaopuuzia elimu hiyo, kutokana na jinsi walivyoelekezwa tangu mwanzo ulipoingia ugonjwa huo nchini.

Jambo la muhimu tunaloamini, ni jamii kupata elimu sahihi na kuachana na hayo nyingine ya mitaani, ambayo unalenga kupotesha na kusababisha watu kuendelea kuumia badala ya kujikinga.

Pamoja na hayo, tunashauri kupanuliwa kwa wigo wa utoaji wa elimu kwa kushirikisha hata vyama vya siasa, kwani navyo vina wafuasi wengi ambao hukusanyika kwenye mikutano ya hadhara.

Viongozi wa vyama hivyo wanaweza kutumia nafasi hiyo kutoa elimu kwa wafuasi wa vyama vyao, kwani nao wana ushawishi mkubwa unaoweza kusaidia katika vita ya kutokomeza UVIKO-19.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Christina Mwakangale

## Muungwana Lazima Nilonge

# Mgawanyo huu wa kazi kijinsia urekebishwe, usikwaze wanawake

**DHANA** kadhaa kwenye jamii kama mgawanyo wa kazi kijinsi ni kati ya vikwazo vinavyomvuta nyuma mwanamke na mabinti kwenye kujitambua, kuwajibika na kuwa sehemu ya maendeleo, badala yake huwalazimisha kuishia kubeba majukumu ya kulea familia.

Ni kawaida jamii kugawana majukumu kulingana na jinsi hususan kwa Waafrika kwa kutenga shughuli ambazo zinazofanywa na wanawake na za wanaume peke yao kama kuchimba makaburi, kuchinja na kuchuna wanyama.

Mgawanyo huu wa majukumu ni dhana zilizojengwa kwenye jamii kama vile kupika, kuchota maji, kufanya usafi nyumbani, kufua, kuosha vyombo na kulea familia zaidi hufanywa na mwanamke.

Kwa upande wa wanaume imezoeleka tangu wakiwa wavulana kazi zao aidha ni kulisha au kuchunga mifugo, kukata mita, kupasua mbao. Ndilo jukumu la wavulana na anapokuwa mkubwa atatafuta pesa ya kujikimu iwe ni kilimo, biashara na hata kuchimba madini.

Kwa kiwango kikubwa kuanzia vijijini hadi mijini mgawanyo huo wa majukumu, umekuwa ni desturi na wengineko ni kama kanuni au sheria.

Mtoto wa kike ambaye anasoma shule majukumu yake kijinsia yapo palepale, akirudi nyumbani, apike, aoshe vyombo, kuchota maji, kulea wadogo zake, pamoja na ukweli kwamba alihitaji kupunguziwa mzigo ilia pate nafasi ya kusoma kama mvulana.

Msichana, huyu pia ana majukumu mahususi kwa kutokana na maumbile mfano kubeba ujauzito, kujifungua, kuingia hedhi na kunyonyesha ilihali jukumu la wanaume kijinsi ni kutunga mimba.

Mahitaji haya yanamfanya mwanamke kuhitaji rasilimali zaidi za kibajeti kuliko mwanaume, hasa kwa wasichana ambao bajeti yao ya kila mwezi kununua taulo za kike haina mbadala.

Mjadala kuhusu usawa wa kijinsia katika muktadha wa maisha kwenye jamii utaongeza uelewa wa pamoja kuhusu dhana zinazotumika.

Kwenye masuala ya kijinsia na kuongeza weledi wa kina kujua maana na mantiki ya dhana za jinsia hadi maandalizi ya mchakato wa bajeti yenye mrengo wa kijinsia kuanzia ngazi ya familia hadi ngazi za juu kitaifa.

Tofauti ya kimaumbile ambayo ipo kwa mwanamke na mwanaume haibadiliki, ijapokuwa kumekuwa na jitihada za kitaalamu na za kisayansi pamoja na kiteknolojia kubadili maumbile, lakini mabadiliko yanaweza kutokea ya viungo siyo ya maumbile ya asili.

Tofauti katika jinsi ndiko kunakotofautisha majukumu pia kwenye makundi fulani na kuwapo dhana kwamba mwanamke hawezi kufanya shughuli za mwanaume na kusisitiza kuwa zake ni hizi ama zile.

Mahitaji ya kimkakati kijinsia yatawezesha hatua za maendeleo ambayo kila mtu anatakiwa kuyapata katika jamii ili kumkwamua kiuchumi au kijamii lakini kuliwezesha taifa kufikia maendeleo endelevu.

Elimu yenye usawa na yenye mazingira yanayompunguzia mzigo msichana ni muhimu kwa kuhakikisha kila shule ina mabweni ya wasichana pia wanawake wajasiriamali wanapata fursa za kupata mikopo.

Serikali imeliona hili na katika bajeti ya 2021/22 yapo mahitaji ya kimkakati yamezingatiwa kwa kujenga shule za sekondari za wasichana za sayansi katika kila mkoa, kupunguza mimba za utotoni na kuongeza wasichana wanaojiunga vyuo vikuu.

Dhana za mfumo dume usio na sura ya kike kuhodhi madaraka, maamuzi na umiliki wa rasilimali unarudisha maendeleo nyuma katika jamii.

Fursa duni kwa msichana tangu masomoni inakuwa chanzo cha mfumo duni wa maisha yao katika maeneo mengi nchini hasa nafasi za uongozi katika shina wanabakia kuongozwa na wanaume hata kwenye kata, kitaifa na kimataifa hali ni hiyo hiyo, pengo kubwa kati ya wanawake na wanaume.

Mfumo huu jamii isipobadilika unaendeleza sera, sheria na mikakati mbalimbali ya maendeleo na katika nyanja zote za maisha kupitia malezi na makuzi, elimu, mila na desturi.

HABARI KITAIFA

# Mvutano DC, M/kiti sasa waibua mapya

**Na Mwandishi Wetu,** MONDULI

MWENYEKITI wa Serikali ya Kijiji Eng'arooji kilichopo Kata ya Lepurko, Wilaya ya Monduli mkoani Arusha, Ngalama Mapema, 'amemvimbia' Mkuu wa Wilaya hiyo, Frank Mwaisumbe, baada ya kutangaza kumsimamisha kazi.

Mwaisumbe alichukua hatua hiyo kutokana na tuhuma mbalimbali ikiwamo kuhamasisha wananchi kuushambulia kwa mawe msafara wake.

Ngalama amenukuliwa akisema, hoja ya kumsimamisha kazi kwa mujibu wa sheria, wenye mamlaka hayo ya kumuondoa ni wale waliompa ridhaa au Chama cha Mapinduzi (CCM) kilichomdhamini.

Kutokana na sakata hilo, amemshauri Mkuu huyo wa wilaya, mambo mawili anayoweza kuyafanya kwa sasa, kwamba anaweza kuchukua uamuzi wa kumpeleka mbele ya umma wa wananchi wa Eng'arooji na akawahoji kwa mujibu wa sheria, ili wapige kura ya kumuondoa.

"Ni kweli Mkuu wa wilaya na msafara wake ulishambuliwa na wananchi, lakini mimi sijawatuma wamshambulie, ila nikiwa chini ya ulinzi wa Polisi, wananchi ndio walipandwa na hasira, wakitaka nisipelekwe Kituo cha Polisi na kuanza kurusha mawe," alisema.

Aidha, mwenyekiti huyo amedai kuwa hakubaliani na uamuzi uliotolewa wa kusimamishwa uongozi, kwa kuwa mamlaka iliyomuweka madarakani ambao ni wananchi, bado wanamhitaji.

Aliwatuhumu baadhi ya wananchi wake wakiongozwa na mfanyabiashara mmoja wa madini kijijini hapo, ndio wanaoongoza mgogoro huo, baada ya kujimilikisha kinyume cha sheria eneo la kijiji, lenye ukubwa wa hekari 700.

Septemba 29 mwaka huu, DC Mwaisumbe alitangaza kumsimamisha kazi mwenyekiti huyo, kutokana na tuhuma za kuhamasisha wananchi kuushambulia kwa mawe msafara wake.

Kwa mujibu wa Mwaisumbe, Septemba 24 mwaka huu, akiwa na kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya hiyo walishambuliwa kwa mawe na wananchi wa kijiji hicho.

Aidha, Septemba 27 mwaka huu baada ya kutokea kwa tukio hilo, wakazi wa kijiji hicho walikimbilia kwa Katibu wa CCM Mkoa wa Arusha, Musa Matoroka, wakitaka chama kiingilie kati mgogoro huo na kuupatia ufumbuzi.

Akizungumzia mgogoro huo, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, alieleza kusikitishwa kwake na tukio hilo la wananchi kujichukulia sheria mkononi na kushambulia viongozi, huku akiagiza waliohusika na vurugu hizo wachukuliwe hatua.

Alipoulizwa kuhusu agizo hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo, alisema jeshi hilo limeanza uchunguzi na limewahoji watu sita kuhusiana na tukio hilo.

# NMB yaja na hati kiapo cha huduma kwa mteja

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB jana ilizindua maadhimisho ya wiki ya huduma kwa wateja kwa kuahidi kuwahudumia kwa viwango bora vya hali ya juu ili kuendelea kuwa taasisi ya fedha pendwa.

Ahadi hiyo ipo kwenye hati ya kiapo cha huduma kwa mteja ambayo benki hiyo iliizindua sambamba na uzinduzi wa shughuli za wiki ya wateja ambazo kitaifa ilifanyika jijini Dodoma.

Katika hafla hiyo na kama sehemu ya sherehe za kuadhimisha wiki ya huduma kwa wateja, NMB pia ilitoa misaada mbambali mkoani huo yenye thamani ya Sh. milioni 40 yakiwamo madawati na vifaa vya hospitali.

Mgeni rasmi alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, ambapo Ofisa Mtendaji Kuu wa NMB, Ruth Zaipuna, alisema hati hiyo ni maazimio na matamanio ambayo NMB imejiwekea ili kufikia adhma ya kutoa huduma bora, shindani na yenye tija.

Tukio hilo pia lilihudhuriwa na wabunge wa Mkoa wa Dodoma, wakuu wa wilaya tatu za mkoa wa Dodoma, wateja wa NMB na viongozi mbalimbali walioipongeza benki hiyo kwa ubunifu na ubora wa huduma zake huku wakisema uwekezaji inayoufanya katika maendeleo ya taifa ni mkubwa na wa kuigwa.

Zaipuna alisema hati ya kiapo cha huduma kwa mteja ni nyenzo muhimu katika kuweka uhusiano mzuri na wateja wa benki hiyo, ili waendelee kuiamini na iweze kuendeleza ushindani wenye tija sokoni. Mkataba huo wa hiari pia unaiwezesha NMB kuweka maazimio ya uhusiano wa kibiashara wenye afya na wateja wake.

Zaipuna alisema kimsingi hati hiyo ina ahadi tano za benki kwa mteja ambazo ni kupatikana kwake kwa haraka, usikivu, uhakika na kuaminika, usalama wa taarifa za mteja pamoja na weledi na nidhamu.

Akiwapongeza wateja kwa kuiunga mkono benki hiyo na kuchangia mafanikio yake, Zaipuna alifafanua kuwa ahadi hizo ni maazimio yatakayolinda haki ya mteja na pia yenye kudhamiria kudumisha uhusiano wao mzuri.

Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

VACANCY ANNOUNCEMENT

Air Tanzania Company Limited (ATCL) is implementing its five years Corporate Strategic Plan (2017/2018-2020-2021) which includes the network expansion in local, regional and international destinations as well as improvement of its internal operations and human capital management. Therefore, applications are invited from qualified Tanzanians to fill the position of Aviation Security officer.

**1. POSITION : AVIATION SECURITY OFFICER (2POSTS)**

**1.1 JOB SUMMARY:**
To ensure Security and Safety of passengers and luggage from checking up to disembarking as well as maintaining security of equipment directly associated with ATCL operations.

**1.2 QUALIFICATIONS:**
- Minimum Advanced Certificate of Secondary Education
- Must have attended and passed TCAA approved screener course and relevant AVSEC training.
- Must be computer literate
- Certificate in Law or any post-secondary qualification will be an added advantage
- At least three (3) years working experience in Aviation Security
- Must be a Tanzanian

**1.3 RESPONSIBILITIES:**
- Responsible for the ATCL Security Operations.
- Proactively supervise and control security operations station to ensure security of departure and arrival of ATCL flights
- Implement security deployment plan to ensure secure coverage of all areas of operation.
- Ensure proper coordination with contracted aviation service security providers for the entire process of ATCL.
- Build good working relationships with security providing partners to facilitate for timely/immediate solution of any security issues affecting ATCL.
- Ensure contracted aviation security service providers consistently adopt procedures, processes and all other relevant amendments made to the ATCL aviation security program
- Ensure proper handling, carriage and disposal of fire arms and other prohibited items to comply with set standards.
- Undertake checks and vulnerability test for contracted aviation security services to ensure continued standards of work performance.
- Analyze theft, pilferage and loss of baggage trends and develop security counter-measures to ensure security of company, customer and staff properties.
- Conduct preliminary investigation on all detected/reported cases within the scope of aviation security to ensure speedy conclusion.
- Ensure safe collection and forwarding of lost and found properties to the Aviation Security Officer – Standards, Training and Records for hand over to owner or disposal.
- Protect and ensure Company revenue integrity through collection of unpaid excess weight charges.

**2. REMUNERATION:**
Attractive remuneration and Fringe Benefits as per ATCL Scales and Incentive Scheme.

**3. TERMS OF EMPLOYMENT**
Fixed Term Contract of Five (5) years

**4. MODE OF APPLICATION:**
Interested applicants must submit a**signed letter** for consideration of the applications attached with the following:

i. A detailed curriculum vitae (CV);
ii. Certified copies of all certificates (including Secondary School and birth certificate), and other relevant certificates and licenses. **(Tanzanian applicants who have studied outside Tanzania should have their certificates approved by relevant authorities i.e Tanzania Commission for Universities (TCU) or National Examination Council- NECTA))**
iii. Two recent passport size photographs;
iv. Names and addresses of at least two reputable referees;
v. Applicant's reliable contact address, email address and telephone numbers.
vi. The applicant must indicate willingness to work upcountry when need be.

**Note: Misrepresentation of facts and qualifications during application shall warrant legal consequences.**

**5. CLOSING DATES:**
Application letters **dully signed should** reach the undersigned **within 14 days from the first date of this announcement: -**

**MANAGING DIRECTOR & CHIEF EXECUTIVE OFFICER,**
**AIR TANZANIA COMPANY LIMITED,**
**P.O. BOX 543, DAR ES SALAAM**

**5th OCTOBER, 2021**

216492802

# RC aonya watumishi afya wizi wa dawa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WATUMISHI wa afya mkoani Shinyanga, wameonywa wizi wa dawa kuepusha upungufu kwenye hospitali za serikali.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Philemon Sengati, alisema hayo, mwishoni mwa wiki kwenye siku ya maadhimisho ya Siku ya Wazee Duniani, yaliyofanyika mkoani Shinyanga katika Kijiji cha Nyandekwa, Manispaa ya Kahama.

Alisema serikali haitamvumilia mtumishi yeyote wa afya kujihusisha na wizi wa dawa na atakaebainika atachukuliwa hatua kali za kisheria.

"Naagiza Waganga wakuu wa kila wilaya mkoani Shinyanga, mfanye ukaguzi wa dawa kwenye huduma za afya kila robo, ili kuhakikisha dawa za kutosha zinakuwapo hospitalini na kutoa huduma stahiki kwa wananchi bila ya bugudha," alisema Dk. Sengati.

"Natoa onyo kwa wale watumishi ambao watajihusisha na ubadhilifu wa aina yoyote wa dawa kwenye huduma zetu za afya za serikali, waache mara moja na yule ambaye tutakae mbaini tutamchukulia hatua kali za kisheria," aliongeza.

Aliwahikikishia wazee mkoani humo kuwa serikali itaendelea kutatua changamoto zinazowakabili, ikiwamo kuendelea kutenga madirisha yao kwenye huduma za afya, upatikanaji wa dawa za magonjwa pamoja na kuwapatia vitambulisho vya matibabu bure na bima za afya (CHF).

Naye Mratibu wa Shirika la TAWLAE, Eliasenya Nnko, linalojihusisha na masuala ya wazee mkoani hapo, aliipongeza serikali kuendelea kutatua changamoto za wazee zikiwamo huduma za afya, pamoja na kupunguza matukio ya mauaji dhidi yao, huku akiiomba serikali iyatokomeze mauaji ya wazee.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (kulia), akikata utepe kuashiria uzinduzi wa huduma ya uwakala wa malipo ya kodi na tozo za mamlaka mbalimbali ikiwamo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) itakayotolewa na benki hiyo, hadi usiku wakati wa hafla ya uzinduzi wa Wiki ya Huduma kwa Wateja iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. **NA MPIGAPICHA WETU**


**BEST GROUP (T) LIMITED**

Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**NOTISI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa Idhini tuliyopewa na **BANK OF AFRICA** Tunatoa notisi ya siku kumi na nne(14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa mdaiwa aliyetajwa hapo chini, alipe deni analodaiwa na benki hiyo pamoja na riba. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) iliyodhamini mkopo wake kwa **MNADA WA HADHARA.** Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 Asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonesha hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | DHAMANA NA MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | ALISON MBONYO | ALISON HASHIM MBONYO | Nyumba ya makazi yenye Hati ya usajili na.16646LR Kiwanja na.107 kitalu"A" iliyopo Mapinduzi mkoa wa Dodoma | 23/10/2021 |

**MASHART YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugezi Mtendaji**
**Best Group (T) Ltd**
**Alli Hassan Mwinyi Road**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor**
**P.O. BOX 1088**
**Dar Es Salaam.**
**Mob: + 255 715-363537/ +255 765-363537**

**AU**

**Mkurugezi Mtendaji**
**Bank of Africa**
**Head Office,**
**NDC Development House, Ohio street/kivukoni**
**P.O. BOX 3054,**
**Dar Es Salaam, Tanzania.**
**Tel: +255-22-2110104/2111290**
**Fax: +255-22-2113740**

216492901


# Sensa ya nyumba na majengo yaja

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amesema serikali iko katika maandalizi ya kufanya sensa ya nyumba na majengo kote nchini.

Sensa hiyo itafanyika sambamba na Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika Oktoba, 2022.

Akizungumza katika Maadhimisho ya Siku ya Makazi Duniani jana jijini Dodoma, Lukuvi alisema, sensa hiyo itasaidia kubaini idadi na hali ya nyumba nchini, hivyo kuiwezesha serikali na wadau wengine wa maendeleo ya makazi kuchukua hatua muafaka za kuboresha makazi ya watu mijini na vijijini.

"Natoa wito kwa wananchi wote kujitokeza katika zoezi la sensa, maana hili ni zoezi muhimu sana na kuna uhusiano mkubwa kati ya watu na makazi na lengo hapa ni kujua hali ya makazi nchini na upungufu wake sambamba na kujua vifaa vinavyotumika kwenye ujenzi wa nyumba," alisema Lukuvi.

Lukuvi alisema, ni vyema kila mwananchi atambue kuwa, Serikali ya Tanzania kupitia wizara na taasisi zake imefanya juhudi kubwa katika kupunguza uzalishaji wa hewa-ukaa hususan kwa wakazi wa mijini.

Alitolea mfano wa usambazaji wa nishati ya umeme kwa gharama nafuu mijini na vijijini, uhamasishaji wa matumizi ya gesi ya kupikia majumbani, upigaji marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki na kampeni ya kutunza na kuhifadhi misitu na vyanzo vya maji kuwa ni miongoni mwa hatua za kimkakati ambazo zimekuwa zikichukuliwa na serikali zikilenga pamoja na mambo mengine kupunguza hewaukaa duniani.

# NBC yaja na kampeni 'Nguvu ya Huduma zenye Zege Halilali'

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imezindua Wiki ya Huduma kwa Wateja sambamba na kampeni maalum inayofahamika kama 'Nguvu ya Huduma, Zege Halilali'.

Huduma hiyo imetajwa kuwa ni kielelezo na chachu ya utoaji wa huduma kwa haraka na kwa wakati kulingana na mahitaji ya wateja wa benki hiyo.

Katika uzinduzi wa kampeni hiyo ya mwezi mmoja iliyoanza jana, ilishuhudiwa pia na Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Theobald Sabi, kwa kushirikiana na viongozi waandamizi wa mamlaka mbalimbali ikiwamo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), walizindua huduma ya uwakala wa malipo ya kodi na tozo mbalimbali za mamlaka hizo itakayotolewa na benki hiyo hadi usiku.

"Utoaji wa huduma kwa wateja kwa kuzingatia weledi na kwa wakati ndio msingi wa mafanikio kwetu kama benki na kwa wateja wetu. Lengo hasa la kampeni ya 'Nguvu ya Huduma, Zege Halilali' ni kuakisi mkakati huo tukizingatia kwamba, wateja wetu wengi hususani wafanyabiashara hawana muda wa kupoteza. Hivyo sisi kama benki lazima twende na kasi hiyo na ndio sababu kupitia huduma hii wataweza kufanya malipo yao ya TRA na Bandari hadi usiku kupitia Benki ya NBC," alisema Sabi.

Alisema katika kufanikisha dhana hiyo ya 'Nguvu ya Huduma, Zege Halilali', benki hiyo imeendelea kuwekeza zaidi katika huduma za kidigitali, ili kutoa huduma zake kwa haraka na wakati sambamba na kuongeza idadi ya matawi pamoja na mawakala wa benki hiyo kila maeneo mengi hapa nchini.

"Kasi hii ya utoaji huduma inakwenda sambamba na ongezeko la huduma zetu mbalimbali zinazobuniwa kwa kuzingatia mahitaji ya wateja wetu ikiwemo huduma ya NBC Shambani mahususi kwa wakulima pamoja na 'NBC Kua Nasi' mahususi kwa wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo." alisema.

Akizungumzia ujio wa huduma ya uwakala wa malipo ya kodi na tozo kupitia Benki ya NBC, Naibu Kamishna Forodha na Ushuru wa TRA, Godfrey Kitundu, alisema huduma hiyo imekuja wakati sahihi na kwa kiasi kikubwa itawasaidia wafanyabiashara wanaotumia bandari ya Dar es Salaam wanapohitaji kufanya malipo ya kodi na tozo za TRA na Mamlaka ya Bandari hata nyakati za usiku.

HABARI KITAIFA

## Mamia mabinti balehe wanolewa ufundi stadi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

JUMLA ya mabinti rika balehe na kinamama vijana 125 wanasomeshwa na Shirika lisilo la kiserikali la Kiwohede wamehitimu mafunzo mbalimbali ya ufundi katika Chuo cha Ufundi Stadi Mwakata.

Lengo la kutoa mafunzo hayo ni sehemu ya kujikwamua kiuchumi, kupinga mimba na ndoa za utotoni pamoja na ukatili wa kijinsia.

Hayo yalibainishwa na Mkurugenzi wa shirika hilo, Justa Mwaituka, katika mahafali ya 17 ya chuo hicho, na kusema wanasomesha mabinti hao kutoka Ikundi mkoani Singida na Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga kwa ufadhili wa UNFPA, UN Women na KOICA.

Alisema kuwa, mabinti hao 125 waliohitimu mafunzo ya ufundi stadi kati yao 75 wanatoka Halmashauri ya Msalala na 50 wanatoka Halmashauri ya Ikungi na kwamba hilo ni kundi la pili la mabinti walionufaika na mafunzo ya stadi za kazi kama njia ya kujikwamua kiuchumi, kupinga mimba na ndoa za utotoni.

## Kafulila aipa SumaJKT mwezi 1 kasi ya ujenzi

**Na Thobias Mwanakatwe**

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, ametoa siku 30 kwa mkandarasi wa kampuni ya ujenzi ya SumaJKT kuongeza kasi ya ujenzi wa jengo la kuchakata Gypsum au watanyang'anywa mradi huo.

Alitoa agizo hilo baada ya kutembelea na kukagua jengo hilo linalojengwa katika Wilaya ya Maswa, utakaogharimu Sh. milioni 678.8 hadi kukamilika.

Kafulila alisema inashangaza kuona kasi ya ujenzi wa jengo hilo ni ndogo wakati mkandarasi ameshalipwa Sh. milioni 169.7, lakini thamani ya ujenzi hailingani na kiasi hicho cha fedha kwa kuwa hadi sasa liko katika hatua ya msingi.

"Nawapa siku 30 nione mabadiliko, nitarudi baada ya mwezi mmoja kama hali itakuwa ileile tutavunja mkataba," alisema Kafulila.

Kafulila alisema serikali haitakubali kuona mradi huo ambao ni muhimu kwa taifa unacheleweshwa makusudi na itakuwa ikifuatilia kila mara kuangalia maendeleo ya ujenzi.

Kampuni ya SumaJKT iliingia mkataba wa ujenzi wa jengo hilo ambao ulianza Juni 2, mwaka huu na unatakiwa kukamilika Desemba Mosi, mwaka huu.

# TADB, IFAD kuwezesha wakulima wadogo kwa mitaji

**Na Mwandishi Wetu**

MFUKO wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD) na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) wameunganisha nguvu ili kuwawezesha mitaji wakulima wadogo kuongeza uzalishaji wa mazao sambamba na kukuza kipato cha wakulima nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kukutana na Mwakilishi Mkazi wa IFAD Tanzania, Jacquline Machangu, Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Frank Nyabundege, alisema wamekuwa na mazungumzo yenye tija kwa manufaa ya nchi kwa kuwawezesha wakulima mitaji ili wafanye kilimo cha kibiashara.

"Tutaendelea kushirikiana na IFAD katika kuhakikisha wakulima wadogo wanapata mitaji itakayowawezesha kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao, hali itakayochochea maendeleo kwa wakulima na uchumi wa nchi kukua," alisema Nyabundege.

Alieleza kuwa TADB inasimamia Mfuko wa dhamana kwa wakulima wadogo (SCGS) kwa niaba ya Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, fedha zinazosimamiwa na TADB kupitia mfuko wa SCGS ni Dola za Marekali milioni 25 kutoka IFAD.

"Kupitia ufadhili huu TADB imeweza kuwafikia moja kwa moja wakulima wadogo 11,468 na kuwafikia wakulima mmoja mmoja zaidi ya 766,380. Tunashukuru ushirikiano mkubwa ambao IFAD wanautoa kwa serikali na kufanya malengo ya serikali katika kuwahudumia wananchi wake yaweze kufikiwa," alisema Nyabundege.

Alieleza kuwa TADB inaendelea kufanya kazi kuhakikisha malengo ya serikali yanafikiwa ikiwamo kuboresha maisha ya wakulima kupitia kuwawezesha kimitaji. Ili kufikia hayo tutaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali zikiwamo taasisi za kitaifa na kimataifa kama IFAD kwa kupata fedha zitakazowezesha kuboresha hali za wakulima.

"TADB kwa sasa inashirikiana na taasisi 12 za kifedha katika kutekeleza Mfuko wa SCGS ambapo umewezesha kuboresha hali za wakulima wadogo kwa kupata mikopo ya kuendeleza shughuli za kilimo kwa dhamana ya TADB," alisema.

Aidha Nyabundege alieleza kuwa benki yake inatoa mikopo ya kuwezesha uanzishwaji wa viwanda vya kuchakata mazao kuongeza ubora zao kwenye mnyororo mzima wa thamani wa mazao hali itakayomfanya mkulima kupata soko la uhakika la mazao yake baada ya mavuno.

Kwa upande, Machangu alipongeza TADB kwa kazi nzuri wanayofanya kuhakikisha wakulima wanafikiwa na huduma za kifedha ili kuwezesha sekta ya kilimo kupiga hatua.

"Ninaelewa kuwa bado kuna changamoto katika upatikanaji wa fedha, hata hivyo napongeza kazi iliyofanywa na taasisi yenu. Aidha, nimejifunza kuwa kupitia TADB mmeweza kushawishi kiwango cha riba katika sekta ya kilimo kupungua... hii itawezesha wakulima kupata mikopo kwa riba nafuu zaidi," alisema Machangu.

Alieleza kuwa wakulima wadogo Tanzania wanalima ardhi hekta 5.1 na kuzalisha asilimia 85 ya chakula cha nchi na kwamba hii ndiyo sababu IFAD inafanya kazi bila kuchoka na serikali ya Tanzania.

"Ikiwa tunataka kuona Tanzania inamaliza njaa, kutokomeza umaskini, kuboresha maisha ni lazima wakulima wadogo waweze kufikiwa na kupatiwa mikopo ili waendeleze kilimo.



Baadhi ya wakazi wa Kata ya Mangirikiti, wilayani Liwale, Mkoa wa Lindi, wakisafisha eneo ambalo litatumika kujenga shule ya sekondari ya kata hiyo, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Busega yakabiliwa upungufu madarasa 79

**Na Happy Severine,** BUSEGA

WANAFUNZI 13,933 wa shule za sekondari wilayani Busega, Mkoa wa Simiyu wanakabiliwa na uhaba wa vyumba vya madarasa.

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa wilaya hiyo, Gabriel Zakaria, wakati wa hafla ya kuchangia ujenzi wa vyumba vya madarasa, iliyofanyika jana, mjini hapa.

Alisema kuna upungufu wa vyumba vya madarasa 79, viti na meza 3,950 na kwamba matarajio ya wanafunzi watakaojiunga na kidato cha kwanza mwaka 2022 ni 6,442 na kufikisha idadi ya wanafunzi 20,375.

"Kwa idadi hii ya wanafunzi vyumba vilivyopo havijitoshelezi kuwahudumia wote, hivyo hatua ya dharura ni lazima zichukuliwe, ili kuhakikisha wote wanapata nafasi ya kwenda shule," alisema Gabriel.

Aliongeza kuwa katika hatua za awali, madarasa yanayojengwa na yaliyofikia hatua mbalimbali yapo 76, huku mahitaji ya vifaa vya ujenzi, ili kukamilisha bado ni makubwa.

Wakizungumza baada ya hafla hiyo wadau wa elimu waliohudhuria katika hafla hiyo, walisema kuwa ubora wa elimu unaendana na ubora wa miundombinu, hivyo ni jukumu la kila mmoja kuboresha mazingira ya mtoto kupata elimu.

"Serikali ina mchango wake katika kuinua ubora wa elimu na wadau wana mchango wao pia, ili kuunga mkono juhudi binafsi zinazofanywa na viongozi wa serikali, ambao wamewiwa kuhakikisha watoto wanapata elimu bora," Dk. Raphael Chegeni mdau wa maendeleo wilayani Busega.

Aidha, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega, Sundi Mniwe, alisema kuwa bado wanaendelea kukusanya na kupokea michango mbalimbali, ili kumaliza tatizo la uhaba wa vyumba vya madarasa.

"Tuna wanafunzi wengi na ni ukweli ambao haufichiki, kuwa baadhi ya kata bado zina shule zenye majengo yasiyojitosheleza, hivyo zinaelemewa tumelazimika kuanzisha michango, ili kuwezesha baadhi ya kata ziwe na shule mbili za sekondari."

Katika hafla hiyo walipata Sh. milioni 82 pamoja na saruji mifuko 2,286, huku wadau mbalimbali wakiombwa kujitokeza kuchangia maendeleo.

# Wanawake wenye VVU 600 kupima saratani mlango kizazi

**Na Mwandishi Wetu,**
BUKOBA

ZAIDI ya wanawake 600 mkoani Kagera wanatarajiwa kufikiwa na mradi wa uhamasishaji wanawake wanaoishi na Virusi Vya Ukimwi (VVU) kupima saratani ya mlango wa kizazi ifikapo Desemba mwaka huu.

Mkurugenzi wa Habari na Uraghibishi kutoka Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS), Jumanne Isango, aliyasema hayo jana alipokuwa uzinduzi wa mradi huo.

Alisema saratani ya mlango wa kizazi ni hatarishi sana hasa kwa wanawake wanaoishi na VVU na ndio maana wametilia mkazo katika eneo hilo ili kujali afya za wananchi.

"TACAIDS kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Uwezeshaji wa Wanawake, (UN-WOMEN) wanatekeleza mradi wa uhamasishaji wanawake hasa wanaoishi na VVU kuchunguza saratani ya mlango wa kizazi mkoani Kagera wilaya ya Bukoba."

"Huu utakuwa ni mradi wa majaribio lakini tunatekeleza moja kwa moja kwani lengo ni kujali afya za wananchi wetu ikizingatiwa kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye maambukizi makubwa ya VVU,"alisema.

Alisema wanatarajia kuona mwitikio mkubwa kwa wanawake hasa waishio na VVU wakijitokeza kufanya uchunguzi.

"Tumeanza na Bukoba Vijijini katika kata tano ambapo tunatarajia kufikia wanawake 600 kufikia Desemba mwaka huu watakaokuwa wamejitokeza kufanyiwa uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi," alisema.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Bukoba, Moses Machali, alisema watahakikisha kuwa kampeni hiyo inafanikiwa.

"Nasi tuungane na TACAIDS, Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto taasisi nyingine za kiraia ikiwamo ambao wamekuwa mstari wa mbele katika kupambana na saratani ya mlango wa kizazi pamoja na VVU ili siku moja tatizo hili lije kuwa asilimia 0," alisema.

Alisema takwimu zinaonyesha kuwa nchini Tanzania kati ya wanawake 1,000, wenye ugonjwa wa saratani ya mlango wa kizazi ni 50. "Tanzania ndio inaongoza kwa kuwa na wagonjwa wengi wa saratani kwa Ukanda wa Afrika Mashariki huku Kanda ya Ziwa tatizo likiwa kubwa zaidi na hali inaonyesha kuwa wenye VVU ndio walioko kwenye hatari ya kupata ugonjwa huu kirahisi," alisema.

Kwa upande wake, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Shirika lisilokuwa la Kiserikali la AMWAVU ambao ndio watekelezaji wa mradi huo, Gasper Lutainulwa, alisema wanawake waishio na VVU wapo kwenye hatari zaidi ya kupata saratani sababu kinga zao za mwili zipo chini kidogo.

"Tunategemea kuona mwitikio mkubwa kwa wanawake wa Kagera, hivyo tupo tayari kuhakikisha ajenda yetu hii inatekelezeka kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwamo serikali,"alisema.

Awali, Mwakilishi wa Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Safina Yuma, alisema kwa sasa kuna vituo takribani 700 nchini vinavyotoa huduma ya uchunguzi wa saratani bila malipo.

Mratibu wa Programu za UKIMWI na Jinsia kutoka UN-WOMEN, Jacob Kayombo, alisema wametoa mchango wao kwenye mradi huo ili kusaidia juhudi za serikali kukabiliana na saratani hiyo.



Katibu wa Jumuiya ya Wanawake Tanzania wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Shinyanga Mjini, Lucy Enock (kushoto), akiwa na Diwani wa Viti Maalum Manispaa ya Shinyanga, Zuhura Waziri, wakiangalia uchakavu wa mindombinu katika Shule ya Msingi Bugweto Manispaa ya Shinyanga huku wakionyeshana ubao wa darasa ambao umetoboka. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Waziri: Serikali itamlinda mkulima

**Na Mwandishi Wetu,**
KATAVI

NAIBU Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, amesema serikali itamlinda mkulima kwa kuhakikisha kilimo kinambadilisha maisha, kwa kuboresha skimu ya umwagiliaji Usense wilayani Mpanda mkoani Katavi.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan, ametoa Sh. milioni 700 ili kujengwa kwa skimu hiyo na kuboresha uzalishaji wa zao la mpunga linalolimwa hapo.

Bashe aliyaeleza hayo alipotembelea na kukagua skimu ya umwagiliaji ya Usense na Msaginya katika Kata ya Uruwira Wilaya ya Mpanda mkoani Katavi.

Alisema, wameweka mkakati ambao utamlinda mkulima, lengo likiwa ni kuhakikisha wakulima wananufaika kupitia shughuli zao za kilimo.

"Ni dhambi kuwaletea matumaini ambayo hayapo utaratibu uko hivi nimempa mhandisi siku 45 na zabuni iwe imetangazwa, watafanya michakato yao kumpata mkandarasi kwa hiyo hii skimu yenye wakulima 250 haitaanza kujengwa leo, itachukua muda hadi kukamilika ujenzi wake.

Aliongeza kuwa, skimu hiyo itajengwa mfereji mkuu ambao utakuwa na kilomita 8 na mifereji mitano ambayo itakuwa na kilomita 7.5 kwa hiyo wakulima hao wasubiri.

"Nataka kupata majibu katika kipindi kifupi kwamba mkandarasi tayari amepatikana na taratibu zote zinaendelea vizuri, tunataka kila kitu kiwe sawa ili waziri aje kuzindua ujenzi wa skimu hii. Serikali itawekeza fedha hizo Sh. milioni 700 ili kujenga hii skimu ya Usense," alisema.

Aidha, alimwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo, mkoani Katavi, kuhakikisha wakulima waliosajiliwa kwenye skimu hiyo wanapimiwa maeneo yao na kupewa hati ya umiliki wa mashamba, kila mtu awe na hati ya umiliki wa shamba lake ili wawe na uhakika ili wawe na uchungu wa kutunza maeneo yao.

# Tigo yaadhimisha wiki huduma kwa wateja

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Tigo imeanza maadhimisho ya wiki ya huduma kwa wateja mwaka huu, ambayo yameanzia mkoani Dodoma.

Wiki ya huduma kwa wateja ilianza kwa matembezi mafupi katika mitaa ya mji wa Dodoma, baadaye kuelekea katika uzinduzi rasmi wa wiki ya CSW, ambayo ilihitimishwa na chakula cha machana pamoja na wateja waaminifu.

Wiki hiyo vile vile itajumuisha shughuli mbalimbali jijini Dar es Salaam ambapo viongozi wakuu wa Tigo watatoa huduma katika kitengo cha huduma kwa wateja cha miito ya simu (Call Center) kwa saa chache ambapo watashughulikia matatizo ya wateja.

Sherehe za wiki nzima zitaenda sambamba na kauli mbiu ya mwaka huu "Power of Service" ambayo inabainisha jinsi timu ya huduma kwa wateja ilivyoweza kukabiliana na mazingira ya kutoka kufanya kazi ofisini kwenda kufanya kazi nje ya ofisi katika kipindi cha janga la ugonjwa wa Uviko-19.

Akizungumza jana katika duka la Tigo Dodoma, Mkuu wa Idara ya Huduma kwa Wateja, Mwangaza Matotola, alisema wiki itakuwa na maonyesho ya huduma bora za Tigo kwa wateja wake na watoa huduma kwa wateja.

"Mwaka huu tumekusudia kubainisha ukaribu mashuhuri wa kampuni ya Tigo Tanzania kwa wateja wake, na msisitizo wetu katika huduma kwa wateja katika wiki hii ni kwa lengo la kutambua kwamba mawakala wetu wa huduma kwa wateja ni taswira ya biashara yetu. Kutokea pale ambapo tatizo la mteja lilipopokelewa mpaka litakapokuwa limetatuliwa, watoa huduma wetu wa huduma kwa wateja wanafanya kazi kwa bidii kuhakikisha kwamba mahitaji ya kila mmoja yamefikiwa kwa wema na furaha," alisema Matotola.

"Kama ilivyo kwa kaulimbiu ya mwaka huu, katika kampuni ya Tigo tunatilia mkazo katika nguvu ya huduma, jinsi ambavyo tunabadilika kuendana na mabadiliko yatokanayo na Uviko-19... hii ndio sababu kwanini tunasisitiza katika kutoa huduma za kuaminika na zenye ufanisi kwa wateja wetu kila siku, jambo hili lilidhihirishwa na timu yetu ya huduma kwa wateja katika mikoa mbalimbali nchini," alisema Matotola.

Alisema wateja wa Tigo wanahamasishwa kutembelea maduka ya Tigo na kutumia mifumo mingine ya kidigitali wanapokuwa wanahitaji msaada, watahudumiwa na timu ya wataalamu wenye mafunzo.

Sherehe hizo ambazo zitadumu kwa wiki nzima ni matokeo ya jitihada za kampuni ya Tigo kuongeza ushirikiano na wafanyakazi. Zaidi ya ushiriki wa timu ya viongozi wa juu, watoa huduma kwa wateja wote katika maduka ya Tigo na vituo vya call center.

**Akizungumza jana katika duka la Tigo Dodoma, Mkuu wa Idara ya Huduma kwa Wateja, Mwangaza Matotola, alisema wiki itakuwa na maonyesho ya huduma bora za Tigo kwa wateja wake na watoa huduma kwa wateja.**

Nipashe
# TESA
Jumanne Oktoba 5, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI




Ukurasa 12

Babu kuoa vijukuu, kutelekeza kunavyowarudi wanaume wazee


Ukurasa 14

**Wanawake waibuka kivingine, ni baada ya kuanza kuwajibika**

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Wapi machapisho nukta nundu, mafunzo kwa lugha ya alama...

■ Ni swali la wenye ulemavu kwa serikali vita UVIKO-19

SERIKALI inahamasisha Watanzania kuchanjwa dhidi ya maambukizi ya COVID-19, kwenye ofisi, juhudi zinahusisha kutembelea wafanyakazi, kuwahamasisha na kuwachanja.

Kila panapotolewa huduma za afya iwe kituo cha afya, zahanati au hospitali, wafanyakazi wanajitahidi kuchanja watu wengi, pale zoezi linaposuasua hawajatimiza wajibu.

Ndani ya vyombo vya habari corona imeshika kasi vikihamasisha watu kuchanja chanjo ya Johnson Johnson, lakini wakati hayo yakifanyika watu wenye ulemavu wana kilio chao.

Wasioona, wanahisi wamesahaulika, wanahoji viko wapi vipeperushi vyenye maandishi ya nukta nundu kuwaelemisha kuhusu UVIKO-19? Wasiosikia wanashangaa hakuna jitihada za kutumia lugha ya alama kuwafikishia ujumbe huo?

Ndivyo wanavyosema pale Nipashe, inapozungumza na baadhi ya wenye mahitaji maalumu katika Manispaa ya Shinyanga hivi karibuni, wakihisi wenye changamoto hizo wamesahaulika.

Mohamed Ally, anasema wenye ulemavu wamesahaulika katika janga hilo, kwa kuwa hawana elimu ya kutosha ya kujiunga na maambukizi.

"Sisi watu wenye ulemavu hatujapata elimu ya kujinga na virusi vya corona, wala chanjo ya UVIKO-19. Wengi wanafahamu kuwa kuna upotoshaji unaoendelea huko mitaani, na kutokana na hali zetu kama wengine hatusikii wala kuona. Bila ya kupewa elimu na wataalamu kwa lugha ya alama au kusoma nukta nundu hatuelewi kitu," anakumbusha Ally.


Mwenyekiti wa TLB Shinyanga, Michael Petrol (kushoto), akizungumzia hali ya wenye ulemavu na UVIKO-19. **PICHA: MARCO MADUHU**

"Tulitakiwa tuaandaliwe maeneo na vifaa vya kutusaidia, wataalamu lugha ya alama, maandishi na vifaa kuliko kuacha hali ibaki kama ilivyo," anaongeza Ally.

Francisco Bega, ni mdau wa masuala ya watu wenye ulemavu, ambaye ana shule binafsi inayotoa elimu kwa watoto wenye mahitaji maalumu katika Manispaa ya Shinyanga, anasema serikali inapaswa kulipa kipaumbele kundi hilo maalum, kulikinga na janga hilo la ugonjwa wa UVIKO-19, kutokana na hali zao.

"Watu hawa wenye ulemavu ni kundi maalum, ambalo serikali inapaswa kuliangalia kwa ukaribu dhidi ya janga hili na UVIKO-19, pamoja na kuchapisha vipeperushi au vitabu vya nukta nundu, vinavyotoa elimu ya corona, mwongozo wa matibabu yake, masuala ya chonjo na taarifa muhimu kuhusu homa hii ili wasome na kupata elimu vizuri ya kujikinga," anasema Bega.

Anakumbusha kuwa wanaoishi na ulemavu ni kundi lililoko kwenye hatari ya kupata maambukizi ya COVID-19, kutokana na hali inayowalazimu kusaidiwa na watu, lakini kutumia vifaa saidizi.

Kutokana na mazingira hayo baadhi wamekuwa na matatizo yanayochangia kupata maambukizi ya UVIKO 19, kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu Mkoa wa Shinyanga (SHIVYAWATA), Richard Mpongo.

Mpongo anakumbusha kuwa wanachama wake wapo katika hatari ya kupata maambukizi ya UVIKO-19 kutokana na kundi hilo mara nyingi kuhitaji msaada kutoka kwa wasio na ulemavu hasa kuwasaidia kwa kuwashika mikono na huo ndiyo uwezekano wa kupata changamoto.

Anasema mtu mwenye ulemavu siku zote hawezi kushinda kutwa nzima bila ya kushikwa mikono kusaidiwa, kwa ajili ya kupewa msaada, na hivyo kusababisha kuwa hatarini.

"Mimi ni mlemavu sioni mara nyingi nikiwa katika shughuli zangu, nashikwa mikono na watu wengi sana kwa ajili ya kupewa msaada na mshukuru Mungu mpaka sasa kutopata maambukizi ya corona," anasema Mpongo.

**TABU NI KUBWA**

Anaungwa mkono na Mwenyekiti wa Chama cha Wasioona Tanzania Wilaya ya Shinyanga (TLB), Michael Petrol, anasema wamekuwa wakipata tabu sana kujikinga na maambukizi ya corona, sababu ya kutokuwa na uwezo wa kufanya jambo peke yao bila ya kusaidiwa, kutokana na kushidwa kuona.

Anasema serikali inapaswa kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi ili kuwakinga na maambukizi ya virusi hivyo, hasa pale wanapokuwa wakiwapatia msaada na kulazimika kuwashika, wahakikishe wamenawa mikono kwa sabuni na maji tirika, ama kujipaka vitakasa mikono, ndipo wawapatie msaada huo na kuiomba serikali iwaangalie kwenye janga hilo la virusi vya COVID-19, anaongeza Petrol.

Michael Mkanjiwa, ambaye ni mlemavu asiyeona, anasema kutokana na maisha yao kuwa katika hatari ya kuambukizwa UVIKO-19, serikali pamoja na wadau wawapatie msaada wa vitakasa mikono, ili kuwakinga pale wanapokuwa wakishikwa na watu wengine.

Anasema idadi kubwa ya watu wenye ulemavu hali zao za kimaisha ni duni, kutokana na ukosefu wa wa kipato ndiyo maana wanashindwa kumudu kununua vifaa vya kuwak-

INAENDELEA UK.12

ELIMU
NA MICHAEL ENEZA

# Babu kuoa vijukuu, kutelekeza kunavyowarudi wanaume wazee



Ndoa ya babu na mjukuu iliyofungwa Nigeria na kuzua 'balaa'. **PICHA: MTANDAO**

SUALA la kizazi cha vijana wa leo kudaiwa kutowajali wazazi wakiwamo baba zao wazee na wakati mwingine kujitenga nao halikuanzia kwao ila baba zao wanahusika.

Kwa kuangalia kanuni za jadi na za kidini, ambazo kizazi hadi kizazi cha wazee kimekuwa kikizivunja, tatizo la msingi halipo katika eneo hilo bali mabadiliko ya 'tabia uchumi' na mmonyonyoko wa maadili miongoni mwa wanaume ambayo hayaruhusu wao kutawala maisha yao kama ilivyokuwa awali.

Muhimu zaidi katika mabadiliko hayo ni kushuka kwa uchumi wa kijijini kuwa wa kubahatisha, na kazi za kudumu kupatikana zaidi maeneo ya mijini, hivyo kuishi kwa kubangaiza vijijini na mijini kwa wasio na ajira rasmi.

Ugomvi wa kirika (au wa kitabaka) kati ya wazee na vijana wao ni kuwa wengi kati ya wazee hawakuwa au hawakuwa katika mahusiano thabiti na wanawake au wazazi wenzao na wake wa ujana wao ambao ndiyo mama wa vijana hao.

Ni katika hali hiyo ambako kuna wajibu wa kimaadili wa kuwaangalia wazazi kwani baba anadoea kile ambacho mwanawe anampelekea mama yake, anapokuwa ni sehemu ya familia ya huyo mama.

Endapo baba ataondoka na kuanzisha maisha kwingine, mwana wa mama huyo hahusiki na matarajio yake huko alikohamia, kimaadili yeye ni baba anapokuwa na huyo mama mzazi na pengine si zaidi ya hapo.

Kinachogomba hapo ni kuwa kuachana kwa wazazi ni jambo lenye simanzi kwa watoto, na ni nadra sana tatizo kuu litokane na mama na kwa hali yoyote ile utii wa mwana ni kwa mama yake. Ukitokea ugomvi kati ya baba na mama, inabidi baba amsikilize na kumwelewa mama kwani ndiye aliyezaa na kulea watoto.

Kitu ambacho si baba wala si huyo mwana anaweza kukifidia, hivyo nafasi ya mama kwa mwanawe ni ya msingi kimaadili, hailinganishwi na ile ya baba. Akimwacha huyo mama, anakuwa ndugu wa karibu kama wengine, lakini pengine watoto hawamthamini kama baba, wanayewajibika kumsaidia na kuwa karibu naye.

Kuna suala linaloibua mijadala maeneo mbalimbali kuhusu wazee kuoa wanawake wadogo sana kwao, kile baadhi wanachokiita 'ndoa za babu na wajukuu' ambazo mara nyingi si ndoa halisi hasa kwa Wakristo ila mahusiano ya dhati ni nyumba ndogo.

Baadhi ya wazee wanaojadili suala hilo wanasema nafasi ya baba iko pale pale, anastahili misaada ya mwanawe hata kama ameoa 'dogodogo' lakini hali halisi mara nyingi haiko hivyo. Kama anahitaji au angehitaji msaada angebaki nyumbani kwake kwa mzazi mwenzake ambaye mwanawe anahusika, siyo kuanzisha familia mpya.

Mtu anayekaribia kustaafu anapooa msichana anakuwa mshindani wa vijana wanaotaka kuanzisha maisha na msichana huyo aliyeolewa katika ndoa ya babu na wajukuu, kwa mantiki ya kitabaka mzee anayejifungia na kijana mdogo anatoa tangazo la kumudu mahusiano hayo, kivyake.

Hawezi tena atoke nje, avae kofia ya uzee, atake misaada wakati anafurahia unyumba wa ujana pale anapokaa, ni kichekesho, au kipingamizi kimaadili. Kimsingi vijana wanachukizwa baba zao wakijifunga na wasichana wa rika lao, hata wadogo kuliko na kwa vile kila mtu huko huru hawezi kuingilia suala hilo. Ila kuna gharama zake, kuwa baba ajue 'atakula jeuri yake au itakula kwake.' Hivyo endapo kijana hawajali wazee wake wawili wanaokaa pamoja kama mwanzo, anastahili apimwe akili kwani anakaribisha laana, ila kama baba alishaondoka nyumbani, ustawi wake huko hautamhusu.

Anaweza kutoa msaada akiweza au akitaka ila hana wajibu kwa suala hilo kimaadili. Kwa maana hiyo ni sahihi wazee wakafurahia uhuru wa kuoa na kuacha, ila wasitazamie kuwa eti kuna kufaidi msaada wa watoto hata kama waliwazaa na kuwatelekeza.

## Wapi machapisho nukta nundu, mafunzo kwa lugha ya alama...

**INATOKA UK.11**

inga na maambukizi ya virusi vya corona.

"Sisi wenye ulemavu hali zetu za kiuchumi si nzuri, ndiyo maana wengi wetu kama unavyotuona hatuvai barakoa, na ambao wanavaa wamepewa msaada, lakini kama tukipata msaada wa vifaa hivi hasa vitakasa mikono vitatusaidia sana kujikinga na corona, sababu tutakuwa tukipaka muda wote," anasema Mkanjiwa.

"Ninapokuwa na kitakasa mkono mfukoni kwangu, nikishikwa kupewa msaada najipaka, hapo nitakuwa salama zaidi, kuliko hivi sasa hatuna na hata kama wachache wanavyo tunabakia kwenye hatari ya kuambukizwa COVID-19," anaongeza Mkanjiwa.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Yudas Ndungile, anasema wenye ulemavu kweli ni kundi ambalo lipo katika hatari kubwa ya kuambukizwa ama kueneza maambukizi ya ugonjwa wa UVIKO-19, na kubainisha kuwa tayari ameshatoa maelekezo kwa Ofisa Ustawi wa Jamii mkoani humo, kutoa elimu ya kujikinga na corona.

"Maambukizi ya corona mkoani Shinyanga yapo, na watu wanapoteza maisha, na tuna wagonjwa waliolazwa na wapo wanaotumia mitungi ya oksijeni, lakini bado hatujapa idadi kubwa ya watu wenye ulemavu kuugua ugonjwa huu wa UVIKO-19, japo kuwa ni kundi ambalo lipo katika hatari kubwa ya kuambukizwa ama kueneza," anasema Ndungile.

"Kundi hili tusipoliangalia kwa ukaribu, tunaweza kupata idadi kubwa ya wagonjwa wa corona kutokana na hali zao, na sisi kama serikali tutalifanyia kazi, ili kuhakikisha maambukizi hayaenei kwa kasi kupitia kundi hili la watu wenye ulemavu,"anaongeza Ndungile.

Lidya Kwesigabo, ni Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Shinyanga, anasema wameshaandaa mpango huo wa kutoa elimu kwa wananchi, juu ya kuwakinga watu wenye ulemavu na maambukizi ya virusi vya corona.

Dk. Ngungile anataja idadi ya watu ambao wameshapata chanjo mkoani Shinyanga, kuwa ni 6,027 wanawake ni 2,012 na wanaume ni 4,015, kati ya dozi za chanjo 25,000 zilizotolewa mkoani humo.

Kaimu Mganga Mfawidhi katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Shinyanga, Dk. Richard Mhangwa, anasema idadi ya wagonjwa imepungua na kubaki wagonjwa watano na kwamba ni mmoja anatumia oksijeni.

Mratibu wa Chanjo mkoani Shinyanga, Timoth Sosoma, anasema awali walianza kutoa elimu ya corona na chanjo ya UVIKO-19 katika makundi hayo maalum, wakianza na wazee na kubainisha kuwa kundi linalofuata ni watu wanaoishi na ulemavu.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, anawataka wananchi kuwalinda watu wenye ulemavu na maambukizi ya virusi vya corona, hasa pale wanapokuwa wakiwapatia msaada na kulazimika kuwashika mkono, wahakikishe wamenawa mikono au kupata vitakasa mikono.

"Katika ziara zangu ambazo nakutana na wananchi, nimekuwa nikitoa elimu ya kujikinga na virusi vya corona, pamoja na kutembelea kwenye Minada na Masoko, ambapo pia hivi karibuni nitakutana na watu wenye ulemavu kuwapata elimu ya corona na chanjo nikiwa na wataalamu wa afya,"anasema Mboneko.

"Pia nimemwagiza Mganga Mkuu wa Manispaa ya Shinyanga, awatembelee watu wenye ulemavu na kuwapatia elimu ya corona, pamoja na kuwafuata walipo na kuwapatia chanjo ya UVIKO-19, sababu ya changamoto walizonazo, ili kulinda afya zao," anaongeza Mboneko.

ELIMU
NA SABATO KASIKA

# Amani Matungullu: Divisheni ‘ziro’ hadi digrii

- Sasa aibua programu kuwabadili wasomi
- Anaabudu zaidi kujiajiri kuliko kuajiriwa

“KAMA unaishi huna haja ya kukata tamaa hata ukishindwa au kupoteza kiasi gani, jipange utafikia mafanikio,” ndivyo anavyosema Amani Matungullu (29) Mkurugenzi wa Kampuni ya Matungullu’s Product Ltd, inayoendesha programu ya kuwaandaa wasomi kujiajiri.

Katika mazungumzo na Nipashe jijini Dar es Salaam, anakumbusha kuwa alianza kutumbukia shimoni mwaka 2003 alipopata divisheni ‘zero’, alipomaliza kidato cha nne kwenye Sekondari ya Shelui, huko Iramba Singida.

Anataja sababu zilizochangia kupata daraja hilo kuwa ni uhaba wa walimu, shule kuwa mpya na pia wakati anasoma, alikuwa akipiga picha mitaani kusaka ada na kodi ya chumba.

“Haya mazingira kwangu yalikuwa ni magumu sana kwa sababu nilikuwa napenda kusoma na wazazi wangu hawakuwa na uwezo, nikajikuta nikiambulia matokeo hayo,” anasema Matungullu.

**HAKUKATA TAMAA**

Matungullu anasema, hakukata tamaa kusaka elimu, aliamua kuingia Dar es Salaam kwa dada yake, Victoria Godfrey na kuanza kuuza mkaa na ilipofika 2005 alirudia mtihani wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Magomeni Baptist, ili kujipatia alama tatu zinazomwezesha kuingia kidato cha tano, lakini akapata mbili.

Hakukata tamaa, anakumbusha kuwa mwaka 2007 alirudia tena katika Shule ya Sekondari Biafra Kinondoni na kupata krediti tatu na kuanza kusoma kidato cha tano na sita shuleni hapo na kuhitimu mwaka 2009.

Anafafanua kuwa alisoma mwaka mmoja kwa sababu ya ukosefu wa ada na kama mwanafunzi wa QT ilikuwa anaingia darasani jioni.

“Nisingeweza kujiunga na wanafunzi wa kawaida kwa sababu ya ada, sikuwa nayo kwa sababu ya kipato changu kikubwa kipindi hicho ilikuwa ni kuuza vocha barabarani kwenye magari ya kisimama na kwenye mabaa usiku ninapotoka shuleni,” anasema.

**KUGEUKIA ULINZI**

Matungullu alipohitimu kidato cha sita, aliajiriwa na kampuni binafsi ya ulinzi ya Dar es Salaam, akilinda ili kupata riziki na kumudu maisha kwa vile mtaji wa vocha uliishia kwenye kusoma.

Hata hivyo, anasema aliacha kazi hiyo kwa vile ilikuwa ngumu na mshahara kidogo, na kujiajiri kama fundi simu, ujuzi alioupata kupitia fundi aliyekuwa anaishi Mabibo na sasa anaendelea nayo.

“Pamoja na kuwa na hiyo ofisi ya ufundi, safari yangu ya ujasiriamali ilianza rasmi mwaka 2018 baada ya Shirika la kiraia la Mkapani



Amani Matungullu (mbele) akiwa kwenye moja ya madarasa ya kufundisha wanafunzi ujasiriamali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Tunaweza, lilipofika Mabibo kutafuta vijana kushiriki programu ya ujasiriamali,” anasema.

Anasema, alichukua fomu na kuijaza kwa ajili ya kujiunga na mafunzo ya ujasiriamali ya miezi mitatu yaliyoshirilkisha vijana wengi wa kata ya Mabibo na baadaye wakakutanishwa na vijana wa wilaya nzima ya Ubungo na kutengeneza majukwaa ya vijana.

“Majukwaa haya yalikuwa ya ngazi ya mtaa, kata, na wilaya. Mfumo huu ulilenga kuwakusanya vijana pamoja, ili waweze kuwa na chombo cha kusemea changamoto zao ndani ya serikali yao,” anasema.

**KUJIENDELEZA**

Anasema, baada ya hapo aliamua kujiendeleza zaidi kwa kusomea ujasiriamali ngazi za awali hadi kwenye Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo - SIDO kujifunza kuzalisha bidhaa mbalimbali.

“Sikuishia hapo, kwani niliamua kusomea ualimu wa VICOBA kwenye Taasisi ya YEMCO iliyopo Sinza. Kwa sasa mimi mwalimu wa ujasiriamali, mwalimu wa VICOBA na Mkurugenzi wa Matungullu’s Product Ltd,” anasema.

Kwenye suala la elimu, anasema hakuishia hapo, na kwamba hivi karibuni alihitimu digrii yake ya Skoposology ambayo amesoma kwa njia ya online kutoka Mount Zion Institute Marekani.

“Wenzetu wana digrii za aina hiyo ambayo inajikita zaidi kwenye kusudi ambalo mtu amejiwekea kwa ajili ya maisha yake, hivyo wanampa elimu ya kumwezesha kufikia alikokusudia,” anasema.

Anasema, Matungullu kwa sasa inatengeneza bidhaa za usafi zikiwamo sabuni za kufulia, kuoshea vyombo, za chooni, dawa za kusafishia tiles, sink na shampoo, jiki, mafuta ya mgando na pilipili.

“Kwa upande wa bidhaa za chakula, tunatengeneza majani ya chai, viungo vya mchuzi mix, pilau masala, unga wa mbegu za maboga na tangawizi kwa kutimia vifaa ambavyo nimenunua kwa ajili ya kazi hiyo yakiwamo mabeseni,” anasema.

**KUWASAIDIA VIJANA**

Katika maelezo yake anasema, ameanzisha programu iitwayo Matungullu’s Mindsetchanging &Enterpreneurship yenye lengo la kuwaondoa wasomi wanaohitimu vyuo kuachana na fikra ya kuajiriwa, badala yake wajiajiri.

“Ninakutana na wanafunzi wa kidato cha nne hadi cha sita, vyuo na wahitimu na vikundi mbalimbali vya vicoba au vya kuwezeshana na kuvifundisha ujasiriamali wa fikra na vitendo,” anasema.

Anafafanua kuwa ameajiri vijana wanne anaosaidiana, kutoa mafunzo ya kuwaandaa vijana kujiajiri na kwamba, kwa wanafunzi wa kidato cha nne, huwafuata kipindi cha likizo huongea na walimu na wazazi wao, wawaruhusu kuhudhuria programu, huku walimu wakitoa majengo ya kufundishia.

“Kwa wanafunzi wa kidato cha sita wanaojiandaa kwenda vyuoni huwa tunatumia muda wao baada tu ya kumaliza shule wakati wanaposubiria vyuo vifunguliwe ndipo tunawaanzishia hii programu,” anasema.

**KUJIVUNIA MAFANIKIO**

Anasema, tangu aanzishe programu hiyo miaka mitatu iliyopita, imeanza kuleta matokeo chanya kwenye jamii, kwa kuwa tayari vijana watatu sasa wanamiliki kampuni za kijasiriamali ambazo wao ni wakurugenzi.

“Hawa ni kati ya vijana waliohitimu vyuo na kusubiri kuajiriwa na wengine ambao hawakufanikiwa kuwa na elimu ya juu, lakini kwa sasa wanaitwa wakurugenzi wanamiliki kampuni za kijasiriamali,” anasema. Anafafanua kuwa kwa kutumia programu hiyo ameweza kuwafikia vijana 552 kinamama 68 mikoa mitatu hadi sasa, ambayo ni Pwani, Dar es Salaam na Singida, na kwamba anaendelea atafikia mikoa mingne kadri inavyowezekana.

“Kule Kibaha Pwani, kuna kijana anaitwa Kisagasi Amir, yeye ni Mkurugenzi wa kampuni ya Akim Product ambayo ameanzisha mwenyewe, huku msaidizi wake akiwa ni Said Muhindi, Salum Njola ni Ofisa Masoko,” anasema.

Anafafanua kuwa, Mwanza yupo Jesca Gunewe ambaye ni Mkurugenzi wa kampuni ya Kingdom Shine ya ufugaji wa kuku na bata, huku Dar es Salaam akimtaja Felister Sule ambaye ni mkurugenzi wa mgahawa wa chakula.

**TAMBO ZA WANUFAIKA**

Mmoja wa vijana waliofaidika na programu hiyo Jessica Gunewe, anasema, wakati umefika sasa vijana hasa wa kike kuondokana na fikra za kutaka kuajiriwa, badala yake wajipange kujiajiri.

“Ninashauri hivyo kwa sababu asilimia kubwa ya mabinti wanapata changamoto nyingi hasa wanapotafuta ajira mara baada ya kuhitimu vyuo na mwisho wake wanaweza kujikuta wakiangukia kubaya,” anasema Jesca.

Anasema, amehitimu kidato cha nne katika Sekondari St. Elizabeth mjini Morogoro mwaka 2009 lakini matokeo hayakuwa mazuri akaamua kurudia mitihani.

“Baada ya kurudia mitihani nikafaulu, lakini bahati mbaya baba akafariki nikawa sina jinsi ikabidi nisome vikozi vidogo vidogo ikiwamo ya hoteli menejimenti kisha nikafanya kazi hoteli moja huko Zanzibar,” anasema.

Anafafanua kuwa, hali yake kiuchumi bado haikuwa nzuri, akaenda Mwanza akafanya anafanya biashara ndogo, na kwamba kwa kuwa alikuwa akifahamiana na Matungullu akawasiliana naye kupata ushauri.

“Kwa kweli alinisaidia kwa kunifundisha online jinsi ya kufanya biashara kwa kuzingatia ubora na nikawa ninauza juisi katika ofisi mbalimbali hadi mwaka jana nikageukia bata na kuku,” anasema.

Mkurugenzi huyo anasema, alianza kwa mtaji wa Sh. milioni 1.6 akiwa na bata 80 na kuku 1000 aina ya chotara. Hadi sasa ana bata 3000 na kuku 4,000 na wafanyakazi wawili wanaohudumia mabanda ya mifugo hao.

Kwa upande wake Kisagasi anasema, amehitimu kozi ya ufundi wa umeme kutoka Mgulani Vocational Training Centre na kwamba kutokana na ukosefu wa ajira wameamjua kujiajiri kwa kuanzisha kampuni yao ya Akim Product.

“Nilihitimu miaka miwili iliyopita, lakini baada ya kupata mafunzo, sasa tunatengeneza bidhaa kama za Matungullu na kusambaza maeneo mbalimbali ya mkoa wa Pwani,” anasema Amir.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Wanawake waibuka kivingine, ni baada ya kuanza kuwajibika

MCHAKATO wa uwajibikaji unachukuliwa kama utaratibu wa kuwabana viongozi wenye wadhifa kuchukua dhamana ya makosa wanayofanya au yanayotendwa na walio chini yake na ikibidi kujiuzulu.

Pia kiuongozi ni kuwabana wenye dhamana kutimiza wajibu wao kwa umma kama kuwapa wananchi huduma na haki wanazostahili ili kufikia maendeleo.

Hata hivyo, chini ya Mradi wa Uimarishaji wa Ufuatiliaji wa Uwajibikaji Jamii katika sekta ya kilimo na afya (PSA) wilayani Mbozi, dhana ya uwajibikaji sasa inatazamwa kwa upande wa pili, jamii nayo iwajibike kufuatilia na kuweka sawa mipango ya maendeleo. Ikijinyooshea yenyewe kidole kwa kushiriki hatua kwa hatua hadi kujipatia ufumbuzi wa changamoto zake.

Katika kufanikisha uwajibikaji wa wananchi, asasi za kiraia zinashirikiana na wananchi kuimarisha uwajibikajikaji wa kijamii katika kusimamia rasilimali za umma kwenye afya na kilimo kwenye Ukanda wa Kusini mwa Afrika.

Chini ya mradi huo wa PSA, suala la uzalishaji chakula linapewa kipaumbele, katika miradi mingi ya kilimo ikiwamo ya kuwasaidia wanawake wakulima wadogo wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini wakiwamo wa mkoa wa Songwe.

Wilayani Mbozi Mkoa wa Songwe wadau likiwamo Shirika la ActionAid Tanzania na taasisi isiyo ya kiraia ya MIICO, wanawafundisha wanawake wakulima wadogo kuwafuata na kuwatumia maofisa ugani katika shughuli zao za kilimo ili kuongeza tija na chakula kwenye familia.

Haya yanajiri hivi karibuni wakati wa ziara ya wanahabari na maofisa wa ActionAid na MIICO kwenye miradi ya pamoja inayofanyika Mbozi.

Aidha, pamoja na jitihada hizo wanawake wanafunzwa kutunza mazingira na kuzalisha mazao salama kwa afya ya binadamu.

Mafunzo hayo yanayotolewa kupitia mradi wa miaka mitano kuanzia 2019 hadi 2023) wa jamii kuwajibika, unafanywa katika vijiji vya Iyula, Itaka, Zelezeta, Hasamba na Idiwili.

Ukifadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Uswizi (SDC), unahusisha wanawake wakulima wadogo kuwajibika, kufuatilia miradi ya maendeleo, rasilimali na pia kuibua vipaumbele kwenye sekta ya kilimo anasema Samweli Mkwatwa, Meneja wa Mradi wa SDC nchini.

Anaeleza kuwa ili kufanikisha jitihada hizo wanawake wakulima wadogo wa vijiji hivyo vitano wameunda majukwaa yanayotekeleza miradi hiyo.

Akizungumza na Nipashe, mwanajukwaa la wanawake wa Kijiji cha Itaka, Martha Mwasembo, anasema mafunzo ya ActionAid na MIICO ya kuwawezesha kuwatumia maofisa ugani wanaowafunza kulima kisasa, kutumia mbegu, mbolea na viutailifu vya asili na kubadili maisha yao.



Wanawake wa Jukwaa la Zelezeta, waliokusanyika kufuatilia mkutano kuhusu miradi ya kilimo na kutunza mazingira. **PICHA: MWANDISHI WETU**

Anasema maofisa ugani wanawafundisha kuanzisha mashamba darasa au ya mfano. Kwenye mashamba hayo kinamama hao hufunzwa kulima kisasa na majukwaa yote matano yana mashamba hayo ya mfano.

Anasema wanalima mahindi na mazao mengine lakini wanaelemishwa njia bora za kuhifadhi nafaka kwa kutumia dawa za viwandani mfano 'super actellic powder.'

Anasema, "Tunaelimishwa kuhifadhi nafaka kwa kutumia dawa ya 'actelic super' ya unga badala ya ile ya maji ambayo awali hatukufahamu kuwa inaweza kusababisha madhara kama maradhi ya saratani ikihifadhi mazao."

Anaeleza kuwa kupitia mafunzo hayo wanawake kwenye majukwaa wameacha kulima kwa mazoea awali walikuwa wanaona kilimo cha kahawa kuwa ni cha wanaume lakini leo siyo, wanalima na wanamiliki kahawa.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wanawake Kijiji cha Hasamba, Catherine Mponzi, anasema kabla ya kupata mafunzo ya kuwatumia maofisa ugani walikuwa mbali nao wakidhani walikuwa wanashughulikia mazao makubwa kama kahawa, lakini wamefahamu kuwa mahindi, maharage na karanga na mazao mengine ya chakula yanahitaji ushauri kutoka kwa maofisa hao.

Baada ya kuwasaka na kuwatumia wamebaini kuwa ni wajibu wa maofisa hao kuwatembelea, kuwashauri kinamama hao ambao wameongeza uzalishaji baada ya kufuata ushauri, tofauti wa kitaalamu tofauti na siku za nyuma walikuwa wakitumia akili zao na uzalishaji ulikuwa chini.

"Kwa mfano kupalilia nilikuwa sijui unatakiwa kuanza wakati gani, nilikuwa naingia shambani nikiona majani yamekuwa mengi . Kumbe sivyo, kitaalamu ukipanda mahindi baada ya siku 21 unaanza kupalilia bila kujali kuna majani hayapo," anasema Mponzi.

Anasema baada ya kupata mafunzo alilima eneo lenye ukubwa wa robo eka, akipanda mbegu ya asili na kuvuna magunia manne 4.5 ya mahindi, lakini kabla ya mafunzo kwenye robo eka alikuwa anavuna gunia moja au mawili tena akitumia mbegu za kisasa, na kuonya kuwa mbegu nyingi zinazosambazwa kwa wakulima vijijini ni feki.

"Tunaomba wakala wa mbegu wawepo hata vijijini au kwenye kata kudhibiti mbegu kwani wakati mwingine tunauziwa feki jambo linaloongeza gharama na hasara kwa mkulima," anasema.

Wanawake wa majukwaa yote wanazungumzia kuanzisha miradi ya kujikomboa kiuchumi, ikiwamo kulima kahawa na kumiliki zao hilo lililokuwa linatajwa kuwa ni la wanaume kwa vile wanawake hawakugusa mapato yake licha ya kuzitunza na kuzichuma na kuzikausha. Wanafuga wanyama wadogo kama samaki, simbilisi, sungura, nguruwe na kuku kuongeza kipato.

### KUSHIRIKI MIKUTANO

Awali walikuwa hawawajibiki kushiriki mikutano ya vijiji na vitongoji. Wanasema walikuwa mbali na mikutano ya hadhara. Hawakujua kuwa iliwahusu ili kueleza kero zao, kuibua vipaumbele ambavyo hufikishwa kwenye halmashauri kuandaa mipango ya maendeleo na kuwekewa bajeti.

"Mafunzo haya kwenye majukwaa yetu yameamsha sauti ya wanawake. Hata kwenye mikutano ya serikali na vijiji viongozi wa majukwaa ya wanawake wanaalikwa kuhudhuria vikao, tunapigiwa simu na kukumbushwa kuhudhuria," anasema Violet Mkono, Mwenyekiti wa Jukwaa la Itaka.

Mafunzo ya SPA yameamsha ari ya kuhudhuria mikutano kwa wingi na kuibua vipaumbele katika shughuli zao za kilimo na kuviwasilisha kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi na baadhi vimekubalika na kutengewa bajeti ya utekelezaji.

Baadhi ya hoja zinazoibuliwa ni kukosekana maofisa ugani wa kutosha vijijini, kwa mfano Kata ya Iyula yenye vijiji sita ina ofisa ugani mmoja anayehudumia kata hiyo, anasema Mtendaji wa Kijiji cha Iyula Witson Sankwa.

"Tuna vijiji vya Iyula, Idundo, Ipyana, Katate, Igale na Iyula B, lakini ofisa ni mmoja, kinamama hawa wanapaza sauti na hili limezingatiwa na serikali imeahidi kuwangeza," anasema Sankwa.

Pia wana uwezo wa kufuatilia bajeti ikiwamo kukagua fedha zinazoelekezwa kwenye sekta ya kilimo, kitu ambacho hakikuwapo miaka ya nyuma.

Aidha, wanawake wakulima wadogo wanafunzwa kanuni za afya, haki na usawa wa kijinsia misingi ya ufuatiliaji raslimali za umma, uwajibikaji, upangaji, mgawanyo na simamizi wa matumizi ya rasilimali, utendaji, ufanisi na maadili.

Mafunzo yameleta mabadiliko chanya kwa wanawake katika vijiji vyote vitano ikiwamo kuongeza uzalishaji, kuwapo uwajibikaji, kutumia wataalamu mfano maofisa ugani na pia kusambaza elimu hiyo kwa kuwafundisha kinamama wengine vijijini.

"Kupitia mafunzo hayo, wakulima wadogo vijijini wameanzisha vyama vya kuweka akiba na kukopa katika vijiji vyao. Wanachama wananunua hisa na kupata mikopo kwa ajili ya kilimo na miradi mingine ya kujiongezea kipato," anasema, Ofisa Mradi wa PSA, Gloria Mdindile.

Anaongeza kuwa vikundi 52 vya kinamama vyenye wanachama 1,560 katika vijiji vitano wanalima kilimo cha ikolojia kinachotumia mbolea, mbegu na viuatilifu asilia hivyo kuhifadhi mazingira.

Aidha, vikundi vya wanawake kutoka vijiji vitano vimenufaika na mikopo yenye thamani ya Shilingi milioni 16 inayotolewa na Halmashauri ya Mbozi kwa ajili ya wanawake, vijana na wenye ulemavu, kundi hilo likiwekeza kwenye kilimo ikolojia.

### KUTETEA HAKI ZAO

Wanawake wanasema mradi huo umebadilisha maisha yao kwa mfano uhamasishaji wa kujitambua na kupambana na unyanyasaji umewainua wajane kufika mahakamani kudai haki zao walizopokonywa baada ya kufiwa na waume.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Itaka Violet anatoa ushuhuda kuwa mgogoro wa kurithi mali za mumewe ulisababisha afike mahakamani kudai haki zake. "Ilikuwa ni jambo lililoshangaza jamii lakini nilikwenda kuwafikisha baadhi ya wanafamilia waliotaka kuchukua nyumba, mifugo na ardhi ya mume wangu," anasema.





# Mpango waleta kasi ya chanjo ya corona

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UTEKELEZAJI wa mpango harakishi na shirikishi kwa jamii kuhusu chanjo ya Uviko-19, umeshika kasi jijini Dodoma, ambapo hadi sasa watu zaidi ya 13,000 wamechanja.

Mpango huo ambao umeanzisha kampeni ya 'Ujanja ni Kuchanja' unalenga kutoa elimu kwa wananchi ili kuwa na mwamko wa kuchanja kwa hiari chanjo hiyo.

Akizungumza jana na wananchi wa Kata ya Mkonze jijini hapa, Mtaalamu wa Halmashauri ya Jiji hilo, Dk. Joseph Mdachi, alisema serikali imeamua kutoa chanjo hiyo kwa wananchi wake ili kulinda afya za wananchi na kuzuia vifo vitokanavyo na ugonjwa wa corona.

Dk. Mdachi alisema kuwa chanjo ya Uviko-19 ni kama chanjo nyingine zinazotolewa nchini.

"Chanjo hii inatolewa kwenye vituo vilevile na watoa huduma ni wale wale na inahifadhiwa kama chanjo nyingine. Serikali imeamua wananchi wake wapate chanjo hii ili kupunguza na kuzuia kabisa maambukizi na vifo vitokanavyo na ugonjwa wa Uviko-19 nchini," alisema.

Akizungumzia usalama wa chanjo hiyo, alisema kuwa chanjo hiyo ni salama.

"Serikali imejiridhisha kwa kufanya utafiti na kujiridhisha kuwa chanjo hiyo ni salama ndiyo iliruhusu iingie nchini na Watanzania waweze kuchanja," alisema.

Aliongeza: "Dodoma hii watu takribani 13,000 wamechanja chanjo hii, watu hawa tunawafahamu kwa majina. Tunapochanja tunafuatilia kama kuna aliyepata shida au madhara kutokana na chanjo hiyo."

"Nataka niwahakikishie hakuna mtu aliyepata madhara baada ya kuchanja kwa Halmashauri yetu ya Jiji la Dodoma," alisema.

Mtaalamu huyo alisema kuwa yupo kwa ajili ya kutoa elimu na kufafanua maeneo ambayo wananchi watakuwa wanahitaji ufafanuzi juu ya chanjo.

"Mimi na wataalamu wenzangu tunawashauri mchanje kwa sababu ugonjwa wa Uviko-19 unakuja kama wimbi. Ndugu zangu mkiona hadi Rais wa nchi anakwambia chanja, wewe chanja. Usisubiri wimbi lingine, wimbi linapotokea hewa ya 'Oxygen' ni shida kuipata," alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Mtaa wa Chinyika, Kombo Ally Kombo, alishukuru serikali kwa kusogeza huduma ya chanjo hiyo kwa wananchi.

## Maelfu wahitimu wa vyuo wapewa elimu ujasiriamali

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

VIJANA 2,000 wahitimu wa vyuo mbalimbali nchini wamepatiwa mafunzo ya ujasiriamali, ikiwamo ufugaji kuku yaliyotolewa na kikundi cha vijana cha Tusumke jijini Dodoma.

Mwenyekiti wa Kikundi cha Tusumuke, Chritopher Dioniz, alisema hayo alipokuwa akitoa taarifa ya kikundi hicho kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Bunge, Kazi, Ajira na Vijana, Jenista Mhagama.

Alisema kikundi hicho kimefanikiwa kutoa elimu kwa makundi ya vijana mbalimbali wahitimu wa vyuo vikuu nchini pamoja na wanawake na watu wenye ulemavu wanao jishughulisha na ujasiriamali.

"Pia tumeweza kutoa elimu ya ujasiriamali ndani ya Mikoa sita ambayo ni Dodoma, Mtwara, Kigoma, Simiyu, Dar es Salaam na Mwanza na hivi sasa baadhi ya wanakikundi wapo Bagamoyo wakitoa mafunzo ya ujasiriamali," alisema Dioniz.

Aidha, alisema kikundi hicho bado kinakabiriwa na kero mbalimbali ikiwamo ukosefu wa fedha.

"Kikundi kinachangamoto kubwa ya kifedha, kikundi chetu baada ya kupokea fedha ya mkopo kutoka Halmashauri ya Jiji sehemu kubwa ya fedha Sh. milioni 25 zilitumika katika kukamilisha jengo hili. Awali tulikuwa tumekodi eneo la uendeshaji ambao gharama ilikuwa ni kubwa."

Alisema kutokana na hali hiyo, wanashindwa kumudu malengo kwasababu ya bajeti ili kuendelea kutekeleza mradi huo wa ufugaji na uuzaji wa vifaranga.

"Kwani tumekuwa tukiagiza mayai kutoka mikoani na baadhi ya wafanyabiashara wa mayai ambao wamekuwa sio waaminifu wanatuuzia mayai yaliyoharibika na kutupatia hasara kubwa, hivyo tunaamini endapo tukipata kiasi cha Sh. milioni 25 au kutupatia mkopo wa vifaranga vya kuku wa mayai 2,000 pamoja na chakula."

Alisema kutokana na soko kubwa walilonalo hivi sasa la kuku, wanashindwa kulimudu kutokana na uwezo mdogo wa uzalishaji walionao.



Mwenyekiti wa Kikundi cha Vijana cha Tusumuke cha jijini Dodoma, Christopher Dioniz, akitoa maelezo kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Bunge, Sera Kazi, Ajira na Vijana, Jenista Mhagama, alipotembelea kukagua mradi wa ufugaji kuku unaofanywa na kikundi hicho. **PICHA: PAUL MABEJA**

# NCCR Mageuzi yaiomba serikali Baraza la Wazee

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

JUMUIYA ya Wazee ya Chama cha NCCR-Mageuzi imeiomba serikali kuunda Baraza la Wazee la Taifa ambalo halitafungamana na itikadi ya aina yoyote ya kisiasa wala kidini.

Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Martin Mng'ong'o, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akitoa tamko lao kwa waandishi wa habari ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wazee Duniani.

"Kwa upande wa serikali tulikuwa tunaomba kwanza kiundwe chombo cha kitaifa cha wazee kwa maana ya Baraza la Wazee la Taifa, ambalo halitafungamana na itikadi ya aina yoyote sio ya kisiasa wala ya kidini.

"Hiki kinaweza kuwa ndicho chombo sahihi cha kuwazungumzia wazee, lakini pia ni chombo cha kutoa ushauri mbalimbali kwa ajili ya taifa," alisema Mng'ong'o. Aidha, alisema kupitia chombo hicho hata Rais au kiongozi yeyote atakitumia kufikisha ujumbe kwa wazee.

"Wakati serikali ikiendelea kutafakari kuhusu umuhimu wa kuunda baraza huru la wazee wa Taifa, tulikuwa tunaiomba serikali ya awamu ya sita iyafanyie kazi mambo haya ya msingi," alisema.

Aliyataja mambo hayo ni pamoja na afya za wazee ambapo katika matamko mbalimbali ya serikali imekuwa ikisisitiza kuwa matibabu ya kundi hilo ni bure, lakini kiuhalisia bado wanataabika na gharama za matibabu, hata wale wenye bima.

"Bado kuna dawa nyingi haziko katika bima tunatoa wito kwa serikali kuhakikisha wazee wote wana bima na wanapata matibabu na dawa bure," alisema.

Jambo jingine alisema ni pensheni kwa wazee waliolitumikia taifa katika serikali na kampuni binafsi wamekuwa wanapata usumbufu mkubwa kuhusu malipo yao.

Alisema wanaiomba serikali itunge sheria itakayowafanya waajiri na mifuko ya hifadhi ya jamii kutowapa usumbufu wazee wanaostaafu.

"Lakini thamani ya pesa wanayolipwa iwe inapanda kutokana na hali halisi ya fedha na gharama za maisha zilivyopanda, kwa hiyo kuna umuhimu wa kupitia mara kwa mara viwango vya malipo ya wazee," alisisitiza.

Pia mwenyekiti huyo alisema suala jingine ambalo serikali inatakiwa kulifanyia kazi ni matunzo ya wazee katika makambi.

"Tanzania inayo makambi ambayo yanawahifadhi wazee waliokosa watoto wa kuwalea au hawana uwezo wa kuwalea... kiukweli yale makambi hayana hadhi ya utu wa binadamu na wala hakuna huduma za kitaalamu," alisisitiza.

Vilevile, aliiomba serikali iliangalie jambo hilo kwa umakini ambapo Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) unaweza kutumika kuboresha makazi na kuajili wataalamu wa kutunza wazee.

Akizungumzia kuhusu tahadhari ya ugonjwa wa corona, alisema wazee wanapaswa kuelewa kuwa ugonjwa huo upo na waathirika wakubwa ni kundi hilo.

"Tunawashauri wazee wote wachukue tahadhari zote ikiwamo kuchanja, kuvaa barakoa kila wanapokuwa kwenye mikusanyiko ya watu na kunawa mikono kwa maji tiririka. Tunashauri na kusisitiza kwa wazee kama huna sababu kubwa ya kukufanya utoke nyumbani ni busara kupumzika nyumbani," alisema.





# Wanaume watakiwa mstari wa mbele chanjo corona

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANAUME wameshauriwa kuwa mstari wa mbele kwenda kupata chanjo ya kujikinga na ugonjwa wa corona kutokana na ugonjwa huo kuwa na uhusiano na upungufu wa nguvu za kiume endapo watapata maambukizi.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki jijini Mbeya na Ofisa Mwandamizi wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba nchini (TMDA) kutoka Makao Makuu, James Ndege, wakati wa mafunzo kwa waandishi wa habari wa Mkoa wa Mbeya kuhusu chanjo ya corona.

Mafunzo hayo ambayo yalikuwa yanalenga kuwajengea uwezo waandishi wa habari kuhusu umuhimu wa chanjo ya corona inayoendelea nchini kwa sasa yaliandaliwa na Shirika lisilokuwa la kiserikali la ELIMISHA na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya.

Ndege alisema mtu akiambukizwa virusi vya corona vinaathiri mfumo wa mzunguko wa damu na kusababisha baadhi ya viungo kutofikiwa na damu ipasavyo vikiwamo viungo vya uzazi kwa mwanamume.

"Mirija ya damu ni miongoni mwa maeneo yenye vishikizo vya virusi vya corona, sasa mwanamume akiambukizwa anakuwa na uwezekano mkubwa wa kupata tatizo la nguvu za kiume kwa sababu damu inakuwa haifiki kisawasawa kwenye uume," alisema Ndege.

Alisema ili kujihami na tatizo hilo ni vyema wanaume wakawahi kupata chanjo kwa kuwa kwa mtu aliyechanja ikitokea akapata maambukizi anakuwa na uwezekano mdogo wa kupata madhara hayo.

Kwa upande wake Mratibu wa Matibabu, Udhibiti na Kinga wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Shaban Hamada, ambaye alikuwa anatoa elimu kwa waandishi, alisema chanjo ya corona ni muhimu kila Mtanzania mwenye sifa achanjwe.

Alisema chanjo hiyo inamwepusha binadamu kupata maambukizi kwa zaidi ya asilimia 80 na kwamba hata akipata hawezi kupata madhara makubwa kama ambaye hajachanjwa.

Vilevile, alisema chanjo hiyo inaepusha vifo kwa zaidi ya asilimia 90 na kuwataka wananchi kuendelea kujitokeza kwa wingi kwenye vituo vya kutolea chanjo hiyo ili waepuke madhara ya ugonjwa huo.

"Kinga ni bora kuliko tiba, tunahamasisha wananchi kujitokeza kupata chanjo hii ambayo inatolewa na serikali bila gharama yoyote hivyo ni vizuri watu wajitokeze kupata chanjo," alisema Dk. Hamada.

Aliwaomba waandishi wa habari kusaidia kutoa elimu kwa jamii ili kuhakikisha kila mmoja anashiriki kwenye vita dhidi ya ugonjwa huo ambao umetikisa dunia kwa kipindi cha miaka miwili.

Alisema chanjo hiyo ni salama kwa binadamu na imeshathibitishwa na wataalamu kuwa haina madhara na hivyo akawataka wananchi kuacha kuwasikiliza watu wanaopotosha huku wakiwa hawana elimu yoyote kuhusu masuala ya afya.

Mkurugenzi wa Shirika la ELIMISHA, Festo Sikagonamo, alisema shirika hilo liliamua kuandaa mafunzo hayo ili kuwaongezea uelewa waandishi wa habari kwa madai kuwa baadhi wamekuwa wakiandika habari bila kuwa na uelewa kuhusu baadhi ya mambo.

Alisema Shirika hilo litaendelea kushirikiana na serikali kwenye kampeni mbalimbali pamoja na utoaji wa elimu kuhusu mambo mbalimbali ya kijamii na kwamba kwa sasa wanaendelea kuandaa mafunzo kuhusu chanjo ya corona kwa makundi mbalimbali ya jamii.



Baadhi ya wajasiriamali wa soko la Soweto jijini Mbeya wakiendelea kuuza viazi katika soko hilo ambalo ni miongoni mwa masoko ambayo yanaboreshwa kupitia mpango wa Agri Connect chini ya ufadhili wa Umoja wa Ulaya. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Taasisi za dini zashauriwa kuanzisha miradi

**Na Nebart Msokwa,** SONGWE

TAASISI za dini nchini zimeshauriwa kuanzisha miradi itakayowasaidia Watanzania kupata ajira zitakazowaingizia kipato kwa lengo la kuinua uchumi wa jamii na taifa kwa ujumla hali ambayo itachangia amani na utulivu.

Rai hiyo ilitolewa na Askofu Mkuu wa Kanisa la Tanzania Assemblies of God (TAG), Mchungaji Dk. Barnabas Mtokambali, wakati wa ibada maalum ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa kanisa TAG Bethelehemu Revival Temple lililopo Mlowo wilayani Mbozi.

Alisema taasisi za dini zinao uwezo wa kuanzisha miradi mikubwa ya uzalishaji ambayo itatoa ajira kwa Watanzania na kuliingizia taifa kipato kwa njia mbalimbali.

"Sisi kama taasisi za dini tukiwa wabunifu tunaweza kuanzisha miradi mingi ya maendeleo ambayo itatuingizia kipato na hata kuchangia pato serikalini kwa kulipa kodi, hatuwezi kuendelea kila siku kuomba misamaha ya kodi wakati tukiamua tunaweza kuzalisha na kuisaidia serikali kuingiza fedha," alisema Dk. Mtokambali.

Alisema Kanisa hilo la TAG Bethelehemu Revival Temple lililopo Mlowo wilayani Mbozi linaweza kuwa mfano wa kuigwa kwa makanisa mengine kwa sababu tayari limeanzisha miradi inayoliingizia kipato ingawa bado ni kidogo kulinganisha na uwezo wake.

Mchungaji mwenyeji wa kanisa hilo, Steven Damian alisema kanisa hilo kwa sasa linayo miradi miwili ambayo inaliingizia kipato kwa ajili ya kuendesha shughuli za kanisa lake.

Alisema kanisa lake limeshanunua shamba lenye ukubwa wa zaidi ya ekari 100 ambalo wanalitumia kwa kulima mazao ya aina mbalimbali wanayoyauza na kujipatia fedha.

Aidha, alisema kanisa hilo pia limejenga vibanda vya biashara kuzunguka uzio wa kanisa ambavyo vimekodishwa na kuliingizia kanisa zaidi ya Sh. 2,000,000 kwa mwaka.

Wakizungumzia ujenzi wa kanisa hilo, baadhi ya viongozi walisema wamejenga jengo la kisasa la kanisa lao kwa fedha zilizotokana na michango ya waumini wao.

# Madereva mabasi abiria walalamikia ratiba ya LATRA

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

MADEREVA wa mabasi ya abiria kati ya Dar es Salaam na mikoa ya Mbeya na Songwe wamelalamikia ratiba mpya ya usafiri wa mabasi hayo ambayo imetolewa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), wakidai kuwa haiendani na hali halisi ya muda wa kuwasili kwenye vituo vyao vya mwisho.

Wakizungumza na gazeti hili katika kizuizi cha Polisi cha Igawa mkoani Mbeya, madereva hao walisema baada ya kituo kikuu cha mabasi cha jijini Dar es Salaam kuhamishwa kutoka Ubungo kwenda Mbezi, safari yao imepungua na foleni iliyokuwa ikiwapotezea muda mwingi, lakini LATRA imetoa ratiba mpya ambayo imerefusha muda wa kufika katika kituo cha mwisho.

Mmoja wa madereva hao, Timotheo Nyagile, alisema hatua hiyo ya LATRA inawasababishia usumbufu kwa kuwa kuna wakati wanalazimika kusimama na abiria maporini wakisubiri muda waliopangiwa kufika kwenye vituo vya ukaguzi ufike.

"Sasa hivi baada ya stendi kuhamia Mbezi safari yetu imepungua, lakini LATRA wametuongezea muda wa kufika kwenye vituo vya ukaguzi, jambo ambalo linasababisha tufike mapema na kupigwa faini, hali hii inatulazimu tusimamishe magari porini kusubiri muda ufike, tunaiomba LATRA ipitie upya ratiba yake," alisema Nyangile.

Dereva mwingine Juma Abdul alisema ratiba hiyo mpya ya LATRA pia inahatarisha usalama wao na abiria kwa vile inawalazimisha kufika usiku mwingi kwenye vituo vyao vya mwisho wa safari.

Alisema mara nyingi muda wa jioni unapofika malori mengi huingia barabarani na baadhi ya madereva wa malori huwa wamelewa na kusababisha hatari kubwa ya kupata ajali.

"Kwa mujibu wa ratiba hii tunalazimika kufika usiku sana kwenye vituo vyetu vya mwisho, lakini ukizingatia kuwa barabara hii ya Mbeya ni nyembamba na usiku malori mengi huingia barabarani ambapo baadhi yao huwa wamelewa na hivyo kuhatarisha usalama wa abiria," alisema Abdul.

Baadhi ya abiria walisema ratiba mpya ya LATRA sio rafiki kwao kwa vile wakati mwingine inawalazimu kulala njiani bila kuwa na sababu za msingi.

Alex Muibrania alisema kwa abiria wanaolazimika kuunganisha usafiri kwenda majumbani kwao inabidi kulala kwenye vituo vya mabasi kusubiri usafiri siku inayofuata kutokana na mabasi kupoteza muda mwingi njiani wakifuata ratiba ya serikali.

"Kwa mfano mtu anaelekea Chunya, analazimika kulala Mbeya Mjini kwa sababu basi linafika usiku, lakini kama ratiba ingekuwa rafiki kwetu ina maana tungefika na kuunganisha magari ya kwenda nyumbani, hivyo tunaongezewa gharama za ziada bila sababu za msingi," alisema Muibrania.

Ofisa Mfawidhi wa LATRA, Nyanda za Juu Kusini, Denis Daud alisema ratiba hiyo mpya imepangwa kwa kuzingatia vigezo na hali ya usalama barabarani.

Alisema chanzo cha malalamiko ya madereva hao ni mwendokasi wanaoendesha magari hayo na kujikuta wanakuwa mbele ya ratiba, jambo ambalo pia ni hatari kwa usalama wao na abiria.



## Sekta ya Utalii Zanzibar yaendelea kuimarika

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Wawakezaji wa Hoteli Zanzibar, Paulo Roso, amesema licha ya dunia kukabiliwa na wimbi la tatu la ugonjwa wa corona, sekta ya utalii Zanzibar inaendelea kuimarika.

Alisema katika kuhakikisha sekta hiyo inaendelea kuimarika Jumuiya ya wawekezaji wa hoteli itaendelea kutoa ushirikiano kwa serikali ili kukuza uchumi wa nchi.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari baada yaa utoaji wa chanjo ya corona kwa wafanyakazi wa hoteli hiyo.

Alisema hivi sasa hali ya uingiaji wageni inaonekana kuwa ya kutia moyo kutokana na Serikali ya Zanzibar kutoa chanjo ya corona kwa wazawa na wageni wanaoingia nchini.

Alisema wageni anaowapokea kwa wingi katika hoteli yake ni kutoka nchini Italia ambao hufika Zanzibar kwa shughuli za utalii.

Mwenyekiti huyo alisema kuwa bado jamii inatakiwa kufahamishwa suala la kujikinga na maradhi ya corona kwa vile dunia imeingia katika janga la maradhi hayo.

Akitoa elimu ya chanjo ya corona kwa wafanyakazi wa hoteli hiyo, Dk. Abdullah Khatibu, kutoka Wizara ya Afya, alisema chanjo zinazotolewa hazina madhara na ni vyema wananchi kuikubali ili kujikinga na corona.

"Chanjo ya corona ipo salama haijaripotiwa kutokea athari kwa makundi yoyote hapa Zanzibar na nje ya Zanzibar," alisema.

Alisema kuna umuhimu mkubwa wananchi kujikinga na kuchanjwa kwa maradhi hayo ambayo yanaonekana kuwa na kasi yanapompata mtu katika mwili na kwamba kuna wajibu wa wananchi kushirikiana na Wizara ya Afya kutokomeza ugonjwa huo.

Kwa upande wao wafanyakazi wa hoteli hiyo waliyopatiwa chanjo ya corona, walisema uamuzi wa uongozi wa hoteli hiyo kuwapa chanjo umewapa nafasi ya kujikinga na maradhi hayo kwa vile sasa wimbi la tatu linaonekana kuwa na nguvu zaidi.

"Awali kulikuwa na uvumi mkubwa kuwa chanjo hizi zina madhara kwa mwili wa binadamu inayotokana na kuganda damu na kusababisha kupoteza maisha wakati jambo hilo halina ukweli kulingana na maelezo ya watalamu," alisema Beatrice Julias Musomi.

# Vizuizi upatikanaji haki za wanawake vyatajwa

**Na Rahma Suleiman**, ZANZIBAR

VIZUIZI vya kitamaduni, kijamii na kitaasisi vinazuia ufikiaji wa haki ya wanawake Zanzibar na sehemu nzuri ya mali ya ndoa baada ya kuvunjika.

Hayo yalisemwa jana na Dk. Yahya Khamis Hamad, Mkuu wa Sheria katika Chuo Kikuu cha Zanzibar (ZU) katika kikao cha uwasilishaji wa utafiti aliofanya kuhusu haki za wanawake na mgawanyo wa mali kwa wanandoa na huduma za watoto.

Alisema kuwa, Sheria ya Mahakama ya Kadhi ya mwaka 2017 ina upungufu ambao unahitaji kufanyiwa kazi ili kuhakikisha mwanamke anapata sehemu yake katika mali ambayo amechangia au kuichuma katika ndoa.

Kwa mfano, alisema sheria haichunguzi vigezo vya mtu kustahili kuwa mpatanishi, lakini haionyeshi malipo halisi ya zawadi ya kuagana baada ya ndoa kuvunjika.

"Lazima kuwe na uamuzi wa malipo ya zawadi ya kuagana na kugawanya mali za ndoa," alishauri Dk. Yahya katika kikao hicho kilichofanyika katika Ofisi za Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Tunguu.

Alisema kulazimisha mwanamke kuwa na risiti ya kuthibitisha mchango wake kwa mali ya ndoa sio sawa na inawanyima wanawake haki zao.

Alisema haikubaliki kwa mwanamke aliyeolewa kunyimwa mali ya ndoa baada ya ndoa kuvunjika.

Naye Dk. Sikujua Omar Hamdan, Mhadhiri kutoka Chuo Kikuu cha Zanzibar, alisema Sheria ya Mahakama ya Kadhi ya mwaka 2017 pia iko kimya kuhusu haki za watoto wakati wazazi wakitengana.

Alisema sheria hiyo haijazungumza utunzaji wa mtoto aliye na mahitaji maalum iwapo wazazi wake watatengana ambayo inasababisha maisha magumu na kunyimwa haki zao za msingi ikiwa ni pamoja na kupata elimu.

Alipendekeza kutungwa kwa sheria mpya ya familia ya Kiislamu ili kupunguza mzigo kwa Mahakama ya Kadhi na kuharakisha kutekelezwa kwa kanuni za mahakama hiyo.

Wadau wa haki za wanawake na watoto na viongozi wa dini, walisema changamoto iliyopo ni matokeo ya utekelezaji mdogo wa Mahakama ya Kadhi inayosababisha wanawake kupoteza haki zao za ndoa baada ya ndoa kuvunjika.

Mkurugenzi wa TAMWA-Zanzibar, Dk. Mzuri Issa Ali, alisema kuwa ripoti hiyo inazingatia Zanzibar kuelewa vyema vizuizi ambavyo wanawake wanakabiliwa na kudai sehemu ya mali hiyo.

Alisema wanawake wanaendelea kunyimwa mali iwapo ndoa itavunjika wakati watoto wanateseka zaidi na kupoteza haki zao za kimsingi.

Kesi 1,457 za talaka zilifunguliwa katika Mahakama ya Kadhi Zanzibar mwaka 2020 ikilinganishwa na mwaka 2019, kesi zilikua 1515 na kesi 1,271 (asilimia 87.2) zilitolewa uamuzi na 186 (asilimia 12.8) bado hazijapata maamuzi.



Askofu wa Kanisa la Moravian Jimbo la Mashariki linaloshirikisha mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro na Zanzibar, Kenani Salim Panja, akikata utepe kuashiria ufunguzi wa Kanisa la Moravian Zanzibar jana, Mwera. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Familia zachangia kuongezeka magonjwa afya ya akili

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MRATIBU wa Huduma za Afya ya Akili Zanzibar, Dk. Suleiman Abdu Ali, amesema hali ya wagonjwa wa akili katika jamii inazidi kuwa mbaya kutokana na baadhi ya familia kuamini imani potofu na kumchelewesha mgonjwa kupatiwa matibabu ya hospitali.

Alisema afya ya akili hutibiwa hospitali na maradhi ya akili yanatibika na sio kutumia waganga wa kienyeji ambapo kufanya hivyo kunamsababishia mgonjwa kupata madhara.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari Kidongochekundu kuhusu siku ya afya ya akili ambayo hufanyika kila Oktoba 10 na ujumbe wa mwaka huu ni "Afya ya akili kwenye ulimwengu usio na usawa".

Alisema takwimu za dunia zinaonyesha kwamba huduma za afya ya akili hazipo kwenye usawa kwa asilimia 75-85, pamoja na kuwa matatizo hayo yanatibiwa.

"Bado kundi la afya ya akili limeachwa nyuma halipewi kipaumbele duniani kote katika mataifa mbalimbali huku takwimu za kilimwengu zinasema asilimia 75 hadi 85 ya makundi hayo yapo nyuma na kuonekana halina umuhimu," alisema.

Alisema ili kujikinga na afya ya akili ni lazima iende sambamba na afya ya mwili ushughulikiaji wake.

Alisema matatizo ya afya ya akili yanatibika na kuitaka jamii kuacha tabia ya kuelekeza zaidi imani za kishirikina na badala yake kuwafikisha wagonjwa hospitali kupata huduma za matibabu zitakazomsaidia kupata unafuu na kupona kabisa.

Naye Mratibu wa huduma za afya ya akili Kanda ya Unguja, Mohammed Sharif Haji, alisema unyanyapaa unapokuwa mkubwa na maradhi ya afya ya akili yataendelea kukua.

Aidha, alisema ugonjwa wa afya ya akili lazima upewe kipaumbele katika kupatiwa matibabu na usipotibiwa utaweza kusababisha afya mwili kutokea.

Alisema endapo jamii itafuata taratibu zote za matibabu bila ya kuchelewa wanapobaini maradhi hayo utapunguza wimbi la watu wa aina hiyo.

Sharifu alisema matumizi ya pombe na dawa za kulevya kupitiliza, huathiri zaidi ubongo na kusababisha kutokea matatizo ya afya ya akili.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

MATANGAZO MCHANGANYIKO

PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA ENTEPRISES FINANCE LIMITED (EFL).
KWA MAWASILIANO ZAIDI
**TUPIGIE:0677 111 333**
**AU 0758 112 332**

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi**
**NO.305/2021**

Ombi la **HADIJA ALLY NG`ADOA** kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **ALLY SAIDI NG`ADOA**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo **tarehe** 28/10/2021 kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukagulia
**Tarehe 04/10/2021**

Tarehe 4/10/2021
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

116491302

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE**
**NO.110 OF 2021**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE DAVID MATHEW ZAKARIA OF DODOMA CITY COUNCIL**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY BERNADETHA FIDELIS MAGERE**
**GENERAL CITATION**
***(Rule 75 of Probate Rules Gn.369 Of 1963)***

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 21 day of 10, 2021.
Dated at Dodoma this 29 day of 09, 2021.

RESIDENT MAGISTRATE
DODOMA URBAN

116491402

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

SHIJA SAHANI LUPI ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T 548 CPF – TOYOTA SPACIO. CHASSIS NAMBA AE1116077886. ENGINE NAMBA 4AFE61190. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: DAR/KIJ/RB/478293/2021.

116491502

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ALLY MOHAMED MALIK** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA NOAH YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 729 DUL** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI **KAH/ RB/496/2021**

1164904020

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya Mwanzo MJINI TANGA**

**Usimamizi wa Mirathi No. 163/2021**

**Ombi la FATUMA KARUNGU ATHUMANI Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu IDDI IBRAHIMU MAKUSUDI**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 18/10/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 27/09/2021.

MAHAKAMA YA MWANZO MJINI TANGA
Sahihi ya Hakimu
MAHAKAMA YA MWANZO TANGA MJINI

1164916020

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GODLUCK RICHARD DAMIAN** amepoteza kadi ya gari namba **T 915 DDZ** na taarifa za kupoteza kadi zimefunguliwa katika kituo cha Polisi Bukoba tangu mwezi Septemba 2021 kwa jalada namba **KAG/BUK/RB/470854/2021.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

116490202

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**GERALD KAGALI**
Anatangaza kupotelewa na cheti cha kuhitimu kidato cha nne index No **S.0426/0057** Mwaka 2002 Shule ya Sekondari Wanging'ombe, kilichotolewa na Baraza la mitihani la Taifa
Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa polisi: **DOD/DOD/RB/462135/2021.**

116490302

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**KELVIN DAUD SANGO anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.1410/0082** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MSALALA SEKONDARI mwaka 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya polisi: **KRU/RB/941/2021.**

116491102

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **MWANTUMU OMARI AKIDA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA HIACE** yenye namba za usajili **T 763 AZS.** Yenye Engine namba **2RZ1654436** na Chassis namba **RZH133100229.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa Polisi: **MUH/RB/2584/2021.**

116492002

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **NDAKI SIMBA LUGANDU** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **BOXER BAJAJ** yenye namba za usajili **MC 773 CHK.** Yenye Engine namba **TVZWKD42355** na Chassis namba **MD2B15BYXKWD91273.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa Polisi: **KOR/RB/397/2021.**

116491902

---

**NYADHI INVESTMENT Co. LIMITED**
**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

**M/MWANZO KISESA - SHAURI LA MADAI Na. 9/2015**
**EVA BERNADO KOLOSO..........................................MDAI**
**DHIDI YA**
**SYLIVANUS JOSEPH KIHAYI................................MDAIWA**
**M/MWANZO YA MKUYUNI - SHAURI LA MADAI Na. 37/2020**
**REBECA AYUBU..........................................MDAI**
**DHIDI YA**
**PASCHAL SILVESTER ..........................................MDAIWA**
**M/MWANZO BUKUMBI - SHAURI LA MADAI Na. 10/2020**
**DIANA IBRAHIM..........................................MDAI**
**DHIDI YA**
**SIMON JOHN..........................................MDAIWA**

KWA IDHINI NA MAMLAKA TULIYOPEWA NA MAHAKAMA YA MWANZO KISESA, MKUYUNI NA BUKUMBI TUNAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI ZA WADAAWA. MNADA UTAFANYIKA MAHALA MALI ILIPO.

| SN | MALI INAYOUZWA | MAHALI | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | NYUMBA | MTAA WA MHANDU KATA YA MHANDU WILAYA YA NYAMAGANA | 5/11/2021 SAA 3 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 2 | BOMA LA NYUMBA | MTAA WA KUZENZA-NYEGEZI MWANZA | 5/11/2021 SAA 3 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 3 | NYUMBA | ILIYOPO KITONGOJI CHA MTAKUJA KATA YA USAGARA WILAYA YA MISUNGWI MWANZA | 5/11/2021 SAA 3 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA:**
1. MTEJA ATALIPA ASILIMIA ISHIRINI NA TANO YA BEI ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA NA ITAKAYOSALIA ATALIPA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE. KUSHINDWA KUFANYA HIVYO MTEJA ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI YAKE YA MSINGI NA MNADA UTARUDIWA TENA.
2. GHARAMA ZOTE ZITAKAZOJITOKEZA BAADA YA KUNUNUA MALI KWENYE MNADA NI JUU YA MNUNUZI.

**MAWASILIANO: 0768-588155.**

116492102

---

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**DANIEL CHRISTIAN RWEGASHA** anatangaza kupotelewa na Basic Certificate in Accountancy (BCA) chenye namba BCA0006265 kilichotolewa na College of Business Education (CBE) 12 November, 2016. Yeyote atakayekiona atoe taaifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/JNI/RB/465456/2021.**

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




Mkuu wa Idara ya Huduma kwa Wateja wa Tigo,, Mwangaza Matotola (kushoto), akikata keki kuzindua Wiki ya Wateja mjini Dodoma jana. Wengine ni Mkurugenzi wa Tigo Kanda ya Kaskazini, Henry Kinabo na katikati ni Msimamizi wa Duka la Tigo lililoko Nyerere Square, Sania Mwilima **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mahakama yafuta kifungo cha miaka 30 cha kubaka

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Rufani Iringa imefuta adhabu ya miaka 30 jela na kuamuru Juma Sembu aachiwe gerezani, baada ya kubaini Jamhuri katika mahakama ya chini ilishindwa kuthibitisha tuhuma, kwamba alibaka mwanafunzi wa miaka 10 .

Jopo la majaji watatu, Jaji Augustine Mwarija, Mwanaisha Kwariko na Abraham Mwampashi lilifikia uamuzi huo baada ya kupitia sababu tatu za kupinga adhabu ya kifungo cha miaka 30 jela na hoja zilizowasilishwa na Jamhuri ikiomba mlalamikaji aachiwe kutokana na mapungufu yaliyojitokeza katika shauri hilo. Mlalamikaji alitiwa hatiani katika Mahakama ya Wilaya ya Tunduru, mkoani Ruvuma na kupewa adhabu ya kifungo cha miaka 30 kwa kosa la kubaka binti wa miaka 10.

Inadaiwa tukio hilo lilitokea Septemba 22, 2018 saa tano asubuhi, maeneo ya Shule ya Msingi Mlingoti. Binti na kaka zake wawili walikuwa wakitoka kwenye masomo ya ziada, walikutana na waliyedai ni mlalamikaji akawasimamisha na kuwataka wasafishe eneo la shule.

Mtu huyo alimtuma binti kwenye jengo jirani akafate dekio, inadaiwa naye alimfata huko, akamvua nguo na kumbaka, binti alitoka akiwa analia.

Kaka zake walimfuata, akawasimulia kilichotokea, wakaenda kumfahamisha baba yao ambaye ni shahidi wa nne, akiwa na watoto wake walimfuata mtu huyo shuleni hawakumuona, wakaenda kituo cha mabasi Mbesa wakamuona na kumtuhumu kufanya tukio hilo.

Mshtakiwa alikamatwa, binti alifanyiwa uchunguzi na ripoti ya daktari ilitolewa mahakamani kama kielelezo, mahakama ya chini ilisema mtuhumiwa alitambuliwa vizuri na mashahidi na ushahidi uliwiana na maelezo yake ya onyo.

Mahakama iliona upande wa Jamhuri umethibitisha kosa, ilimtia hatiani na kumpa adhabu ya kifungo cha miaka 30, alipinga hukumu hiyo Mahakama Kuu, rufani yake ilitupwa.

Katika Mahakama ya Rufani alitoa sababu tatu za kupinga hukumu na kifungo dhidi yake, alidai ,mahakama ilikosea kisheria kumtia hatiani na kumpa adhabu hiyo kwa kuegemea kwenye ushahidi wa Jamhuri peke yake, sababu ya pili, upande wa Jamhuri umeshindwa kuthibitisha kosa, dhidi yake bila kuacha shaka na sababu ya tatu Jaji wa Mahakama Kuu na Mahakama ya chini ilikosea kisheria. Mlalamikaji alijiwakilisha mwenyewe na upande wa Jamhuri uliwakilishwa na Wakili wa Serikali Amina Mawoko.

Wakili Mawoko aliomba Mahakama itilie maanani ushahidi wa mshtakiwa, alikubaliana na hoja kwamba ushahidi wa shahidi wa 1,2,3 kuhusu kumtambua mlalamikaji haukuwa mzito.

Alidai shahidi 1,2,3 walishindwa kufafanua kwa ufasaha nani alifanya tukio hilo, kushindwa kumtambua vizuri mlalamikaji katika tukio kuna uwezekano wa kuwapo makosa katika utambuzi.

"Tunakubali kwamba kesi dhidi ya mlalamikaji haikuthibitika bila kuacha shaka, naiomba mahakama imwachie mlalamikaji, iamuru atolewe gerezani,"alidai Mawoko.

Jopo lilizingatia hoja za upande wa Jamhuri, baada ya kupitia hoja zote ilikubaliana na sababu ya pili kwamba Jamhuri ilishindwa kuthibitisha kosa, bila kuacha shaka.

"Swali ni je, shahidi 1,2,3 walimtambua mlalamikaji kuwa ndiye aliyewasimamisha na kumbaka binti.

Jopo lilisema kwamba wakati mashahidi hao wanatoa taarifa kwa shahidi wa nne, baba yao hawakufafanua mtu huyo alivyo, hawakusema ni mrefu au mfupi, hawakutaja aina ya nguo alizovaa na muonekano wake.

Lilisema kwamba hakuna ushahidi kuwa shule hiyo ilikuwa na mlinzi ama la, Jamhuri hawajaleta ushahidi kama mlalamikaji alikuwa mlinzi wa shule hiyo na kama alikuwa peke yake ama la.

"Sababu ya pili ya rufani ni ya msingi, imekubaliwa, kesi dhidi ya mlalamikaji haikuthibitika bila kuacha shaka, hakuna haja ya kuangalia sababu ya tatu.

"Mahakama inafuta kutiwa hatiani kwa mlalamikaji, adhabu ya kifungo cha miaka 30 jela na inaamuru aachiwe gerezani kama hana kesi nyingine inayomtaka kuendelea kuwa huko," lilisema jopo hilo.

## CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA KAGERA (1990) LIMITED

KCU QUALITY COFFEE
Kagera Cooperative Union

**BID NO: KCU/C/21/004** **TAREHE: 05/10/2021**

## MWALIKO WA ZABUNI

### ZABUNI YA UJENZI WA UKUMBI WA MIKUTANO WA KCU (1990) LTD KATIKA KIWANJA CHA RUMULI, MANISPAA YA BUKOBA.

1. Chama Kikuu Cha Ushirika Kagera kimetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano katika kiwanja cha Chama hicho kilichopo Rumuli, Manispaa ya Bukoba. Inakusudiwa kwamba sehemu ya fedha zitatumika kulipia malipo yanayostahiki chini ya mkataba ambao mwaliko huu wa zabuni unatolewa.
2. KCU (1990) LTD sasa inakaribisha zabuni zilizofungwa kutoka kwa wakandarasi waliosajiliwa na Bodi ya Usajili wa Wakandarasi katika Daraja la Saba na zaidi.
3. Kazi za ujenzi zitafanywa kwa awamu kulingana na makubaliano kati ya KCU (1990) LTD na Mkandarasi. Tafadhali kumbuka kuwa, ujenzi wa msingi tayari umefanywa kwa zaidi ya asilimia 65.
4. Zabuni itakuwa wazi kwa waombaji wote wa Kitaifa.
5. Nyaraka za Zabuni zilizoandikwa kwa lugha ya Kingereza zitatoolewa kwa wazabuni baada ya malipo ya ada isiyorejeshwa ya Tshs 100,000 / =. Malipo yanapaswa kufanywa kupitia akaunti nambari ya 01J1055955001 Jina: KCU (1990) LTD GENERAL ACCOUNT-Benki ya CRDB, Tawi la Bukoba
6. Wazabuni wanaostahiki kupata zabuni wanaweza kupata habari zaidi kutoka Ofisi Kuu ya KCU (1990) LTD
7. Ziara ya kutembelea eneo la ujenzi (site visit) kwa wazabuni itafanyika Jumanne, Oktoba 12, 2021 saa 04:00 asubuhi
8. Zabuni zilizochelewa, sehemu ya zabuni, zabuni ambazo hazitakuwa zimepokelewa, zabuni zisizofunguliwa kwenye sherehe ya ufunguzi hazitakubaliwa kufanyiwa tathmini.
9. Wazabuni wanaombwa kuwasilisha barua zao za maombi ya zabuni pamoja na nyaraka ya zabuni iliyojazwa katika bahasha moja iliyofungwa kwa lakiri kabla ya tarehe 26 Oktoba 2021 saa 04:00 asubuhi. Bahasha iandikwe **"Zabuni ya ujenzi wa Kituo cha Mkutano katika Rumuli Plot, Manispaa ya Bukoba"** iletwe kwenye ofisi kuu ya KCU (1990) na kuwekwa kwenye sanduku la zabuni karibu na ofisi ya Meneja Mkuu kwa anwani iliyoonyeshwa hapa chini.
10. Zabuni zitafunguliwa mara moja mbele ya umma, na mbele ya wawakilishi wa wazabuni watakaohudhuria sherehe ya ufunguzi zitakazofanyika tarehe 19 Oktoba 2021 saa 04:30 katika chumba cha Mikutano cha KCU (1990) LTD.

**Meneja Mkuu**
**KCU (1990) LTD,**
**S.L.P 5,**
**BUKOBA.**

216493102

## HABARI MICHEZO

# PRESHA 'DABI' IMEIPONZA MBEYA KWANZA - KOCHA

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Mbeya Kwanza, Haruna Hererimana, amesema timu yake ingeweza kuibuka na ushindi dhidi ya Mbeya City kama wachezaji wake wasingeingia uwanjani wakiwa na pesha ya 'dabi' hiyo ya jijini Mbeya.

Akizungumza baada ya kumalizika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya juzi, na timu hizo kutoka sare ya mabao 2-2, alisema kipindi cha kwanza wachezaji wake hawakuwa na utulivu kwa sababu kwenye akili zao kulikuwa na neno 'dabi' lililowavuruga.

"Kipindi cha kwanza tulikuwa hatuna utulivu, wachezaji walikuwa na haraka sijui kwa nini, nadhani kwenye vichwa vyao waliweka neno 'dabi'. Yaani wanakwenda kucheza dabi na wenzao wa Mbeya City. Hii ikasababisha wawe na haraka sana.

"Wakashindwa kufanya mipango na kuiga mchezo wa wenzao, kipindi cha kwanza kilipoisha, niliwaambia wasiichukulie kama dabi, bali ni kama mechi nyingine tu, wawe watulivu na kweli tukapata sare baada ya kuwa nyuma kwa mabao mawili," alisema kocha huyo raia wa Burundi.

Naye Kocha Mkuu wa Mbeya City, Mganda Mathias Lule, alisema wachezaji wake hasa mabeki walipoteza umakini, mechi ilipokuwa inakaribia kumalizika.

"Kuna matatizo, tulipoteza umakini hasa kwa mabeki wangu, ukifanya makosa kama yale ni lazima uadhibiwe," alisema Lule.

Mbeya City ilitangulia kwa mabao ya Paul Nonga na Richardson Ngodya, huku Chrispin Ngushi akisawazisha yote mawili ndani ya dakika 10 tu, dakika ya 77 na 86.

UZINDUZI...



Msemaji wa Active Media, Clayton Revocatus maarufu Babalevo, akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi wa Active Media. Kushoto ni Meneja Mkuu wa Kampuni ya The Active, Caroline Muia na Meneja wa Wateja, Shamim David. Active Media itasaidia kuunganisha kampuni na wateja wake kupitia mitandao ya You Tube na Instagram. **MPIGAPICHA WETU**

# Azam yajipa matumaini 'kufufuka' Ligi Kuu Bara

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuambulia pointi moja tu kwenye michezo miwili ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyocheza mpaka sasa, klabu ya Azam FC imesema haina wasiwasi wa kufanya vibaya msimu huu kwa sababu ndiyo kwanza ligi imeanza na bado mapema.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Thabit Zacharia 'Zaka Zakazi', alisema timu yao imepoteza mechi moja na kutoka sare kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo wachezaji wengi kuwa wapya na hawajazoeana na wenzao pamoja na mazingira ya baadhi ya viwanja, kushindwa kutumia nafasi, lakini kudharau baadhi ya wapinzani.

Kwenye mechi ya ufunguzi, Septemba 17, Azam ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Coastal Union kwenye Uwanja wa Mkwakwani, Tanga na Jumamosi iliyopita, ilipata kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa Ushirika, Moshi mkoani Kilimanjaro.

"Bado ni mapema, ligi bado ni mbili. Hata msimu ambao Azam tulichukua ubingwa hatukuanza vizuri, tulianza kwa kusuasua, lakini baadaye tukakaa sawa na kuchukua ubingwa," alisema Zaka Zakazi.

Azam ilitwaa ubingwa wa Tanzania Bara kwa mara ya kwanza msimu wa 2013/14 na hadi leo haijawahi kufanya hivyo tena.

"Wachezaji wetu wengi bado wapya, hata maandalizi ya msimu kuna wakati tulikuwa tunabakiwa na wachezaji wachache, wengi wanakwenda kwenye vikosi vyao vya taifa, kwa hiyo muunganiko bado haujawa sawa, lakini hili walimu wanalifanyia kazi.

"Viwanja vya mikoani navyo vina changamoto, ligi ina udhamini mnono, lakini baadhi ya viwanja vina changamoto kubwa, hasa ikichukuliwa kuwa tuna wachezaji wengi wapya, bado hawajavizoea," alisema.

Alisema kingine ni kwamba Azam ni timu kubwa, hivyo wakati mwingine wachezaji wanazidharau timu wanazocheza nazo, lakini wanachokwenda kukikuta uwanjani ni tofauti.

## Polisi Zanzibar kusajili wapya 8

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Polisi Zanzibar, imedhamiria kusajili nyota nane wapya watakaoitumikia timu hiyo kwa msimu mpya wa Ligi Kuu 2021/22.

Hayo yameelezwa na Kocha Mkuu wa timu hiyo, Ali Mtuli, wakati akizungumza na gazeti hili visiwani hapa jana.

Alisema kati ya wachezaji hao wapya wanaotarajia kuwasajili ni washambuliaji wanne, viungo wa pembeni wawili, kiungo wa kati mmoja pamoja na mlinda mlango mmoja.

Kocha huyo alisema, wachezaji wapya watakaowasajili wanatarajiwa kutoka klabu za Ligi Kuu Zanzibar pamoja na Ligi Daraja la Kwanza Kanda huku wawili kati yao watoka Ligi Daraja la Kwanza Tanzani Bara.

"Tunasajili wachezaji ambao wataongeza nguvu timu yetu, ligi yetu ya Zanzibar imetawaliwa na wachezaji vijana, hivyo lazima usajili wachezaji wanaokwenda na kasi ya ligi yetu, hii itasaidia sana hata timu kufanya vizuri na wachezaji kujiamini uwanjani," alisema.

## Omog kuanza na Geita Gold Mtibwa

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Mtibwa Sugar umesema bado unaendelea na mchakato wa kumtafutia kibali cha kufanya kazi nchini, Kocha Mkuu, Mcameroon Joseph Omog na unaamini ataanza rasmi kukaa katika benchi kwenye mchezo wao ujao dhidi ya Geita Gold FC, utakaopigwa Oktoba 16, mwaka huu.

Mtibwa Sugar imecheza michezo yake miwili ya Ligi Kuu Tanzania Bara ikiongozwa na kocha kutoka kikosi cha vijana na Omog kuishia kukaa jukwaani kutokana na kuchelewa kupata kibali cha kufanya kazi nchini.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mtendaji Mkuu wa Mtibwa Sugar, Sabri Abubakar, alisema Omog alishindwa kuiongoza timu hiyo kwenye mechi mbili walizocheza kwa sababu ya kukosa kibali cha kufanya kazi nchini.

"Tumechelewa kupata ruhusa kutoka TFF kwa sababu kocha Omog alichelewa kuwasili nchini, tumelifanyia kazi na mechi ijayo dhidi ya Geita Gold FC, atakuwapo benchi na kuendelea na majukumu yake," alisema Sabri.

Alisema wamejipanga vizuri na wanatarajia kufanya vizuri kuliko msimu uliopita kwa sababu wamesajili wachezaji wazuri pamoja na kuleta kocha ambaye kwa pamoja watashirikiana kufikia malengo yao.

## ZISIKUPITE

### AURIER KUTUA VILLARREAL

MLINZI wa Ivory coast, Serge Aurier mwenye umri wa miaka 28, ambaye sasa ni mchezaji huru baada ya kuondoka Tottenham Hotspurs, anajiandaa kujiunga na Villarreal ya Hispania. **(L'Equipe)**

### RANIERI KOCHA WATFORD

CLAUDIO Ranieri amekubali kuwa kocha mkuu mpya wa Watford baada ya kuondoka kwa Xisco Munoz juzi, Jumapili, na Muitaliano huyo mwenye umri wa miaka 69, alitarajiwa kutia sani jana, Jumatatu. **(Sky Sports)**

### GONZALEZ ANUKIA CITY

MANCHESTER City wanamfuatilia kiungo wa kati wa Hispania, Nico Gonzalez anayekipiga Barcelona, ambaye hajapewa nafasi ya kucheza kwenye kikosi cha kwanza. (Fichajes)

### SANCHEZ NJIAPANDA INTER

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Arsenal na Manchester United, Alexis Sanchez, hajui mustakabali wake Inter Milan baada ya mchezaji huyo mwenye miaka 32, kuchapisha ujumbe na kisha kuufuta, ambao ulikosoa kitendo cha kukosa muda wa kucheza uwanjani. **(Mirror)**

### ATLETICO WAMTAKA WERNER

KLABU ya Atletico Madrid nayo imeingia kwenye kinyang'anyiro cha kumuwania mshambuliaji, Timo Werner mwenye umri wa miaka 25 anayekipiga Chelsea. **(Transfer Market Web)**

### TOURE AITAKA BARCELONA

KIUNGO wa kati wa Manchester City, Yaya Toure mwenye umri wa miaka 38, ametoa ofa kwa Barcelona wakati huu wakiwa katika changamoto, lakini haijulikani kama raia huyo wa Ivory Coast anataka kucheza au kufundisha. **(Sun)**

### BRUCE KUTIMULIWA NEWCASTLE

MIKE Ashley anajua njia pekee ya kumbadili kocha mkuu wa Newcastle ni kumlipa Steve Bruce kwa kuvunja mkataba wake aliotia saini Julai 2019.**(Chronicle Live)**

### NETZ HAITAKI MAN CITY

MLINZI kinda wa Ujerumani anayecheza katika klabu ya Borussia Monchengladbach, Luca Netz, anadai alikataa uhamisho aliosema "hauna maana" kwenda Manchester City miaka mitatu iliyopita, mchezaji huyo mwenye miaka 18, anasema atawakatalia kwa mara nyingine tena. **(Sun)**

### ZIRKZEE AIFUNGUKIA EVERTON

MSHAMBULIAJI wa Uholanzi, anayecheza Bayern Munich, Joshua Zirkzee, mwenye umri wa miaka 20, amesema alikataa nafasi ya kujiunga na Everton mwaka 2017. **(Het Nieuwsblad via Liverpool Echo)**

### VLAHOVIC KUONGEZA MKATABA

MKURUGENZI wa Fiorentina, Joe Barone, amesema klabu inafanya kila jitihada za kutaka kuongeza mkataba wa nyota wake, Dusan Vlahovic raia wa Serbia, mwenye umri wa miaka 21, ambaye mkataba wake wa sasa unamalizika Juni 2023. **(DAZN)**

### SERGI ATAKIWA MAN CITY

MANCHESTER City inawania kumsajii, Sergi Roberto mwenye umri wa miaka 29 kutoka Barcelona, ambaye mkataba wake unamalizika kipindi cha majira ya joto kijacho. **(Calciomercato)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# GUARDIOLA ASHANGAA MILNER KUTOLAMBWA KADI NYEKUNDU

Lakini hapa Anfield kama ilivyo kule Old Trafford, ingekuwa ni sisi kwa asilimia 100 angetolewa nje...

**LIVERPOOL, England**

PEP Guardiola ameweka wazi kwamba, James Milner, alitakiwa kutolewa nje kwa kadi nyekundu, wakati Manchester City ikitoka sare ya kufungana mabao 2-2 na Liverpool, akiongeza namna gani kikosi chake kilikosa bahati, kwenye mchezo huo.

Akiwa tayari ameonyeshwa kadi ya njano kipindi cha kwanza, Milner aliepuka ya pili ya njano, ambayo ingezaa nyekundu wakati alipomfanyia faulo ya wazi Bernardo Silva, kwenye mchezo huo uliopigwa juzi, Jumapili katika dimba la Anfield.

Tukio hilo lilitokea kipindi cha pili wakati ubao unasomeka 1-1, kabla ya Liverpool iliyokuwa imemkosa Trent Alexander-Arnold kutokana na kuwa majeruhi, kupata bao la pili lililofungwa na Mohamed Salah.

Huku Kevin De Bruyne akiisawazishia City na kuwahakikishia pointi mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu, Guardiola alikuwa na shaka juu ya maamuzi ya mwamuzi, Paul Tierney kwa kushindwa kumuadhibu Milner.

"Ni kadi ya njano," alisema kocha wa City, ambaye akimvaa mwamuzi wa nne, Mike Dean wakati wa mchezo huo na kujikuta akilimwa kadi ya njano, akiiambia Sky Sports.

"Lakini hapa Anfield, kama ilivyo kule Old Trafford. Katika hali hii kama ingekuwa ni sisi na mchezaji wa City akafanya vile kwa asilimia 100, angetolewa nje.

"Ilikuwa ya wazi kabisa. Alifanya faulo iliyoonekana kabisa, lakini hakupewa kadi ya pili ya njano."

Milner pia alihusika kwenye tukio kubwa kipindi cha kwanza, akionekana kumfanyia faulo Phil Foden, jirani na eneo la penalti.

Lakini hakukuwa na faulo, na baadaye mchezaji huyo wa zamani wa City alitolewa nje na nafasi yake kuchukuliwa na Joe Gomez dakika ya 78.

City walitawala kipindi cha kwanza na Guardiola amebainisha kwamba, walikuwa na nafasi nyingi za kufunga, lakini hawakuwa na bahati.

MECHI KALI
HOME
AWAY
MK DONS
2.29 | 3.24 | 2.85
WYCOMBE

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa
halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE
JACKPOT
TZS. 559

# POCHETTINO ASHANGAA PSG KUPOKEA KICHAPO



**PARIS, Ufaransa**

MAURICIO Pochettino aliachwa "amechanganyikiwa na kukatishwa tamaa" baada ya Paris Saint-Germain kushindwa kupiga shuti lolote la kulenga bao, kwenye mchezo waliochezea kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa Rennes, Jumapili.

Vinara hao wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, ushindi wao mfululizo wa mechi nane, ulisimamishwa pale kwenye dimba la Roazhon Park kwa mabao kutoka kwa Gaetan Laborde na Flavien Tait.

PSG walipiga mashuti matatu, lakini hayakulenga goli na walishindwa kumjaribu golikipa, Alfred Gomis, huku Kylian Mbappe akifunga kipindi cha pili, lakini VAR ikalikataa bao hilo kwa kuwa aliotea.

Licha ya uwapo wa nyota wote watatu, Mbappe, Neymar na Lionel Messi, ambaye pia alipiga mashuti matano, moja liligonga mwamba, walishinda kuihakikishia PSG kupata ushindi.

Angel Di Maria alichukua nafasi ya Ander Herrera kutoka kwenye kikosi kilishoshinda mabao 2-0, dhidi ya Manchester City, Jumanne kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini Pochettino hakujutia kuhusu uchaguzi wake wa kikosi.

"Sidhani kama tunaweza kuangalia kuhusu mfumo wa timu yetu. Tulicheza dakika 25 bora kabisa katika kipindi cha kwanza," alisema Pochettino akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Hatukuanza vizuri mchezo, lakini baadaye tulikuwa na dakika 25 au 30 kwa mchezo bora kabisa. Ilikuwa ni aibu kushindwa kupata matokeo."

# Pioli: Wachezaji Milan waote ubingwa Serie A



**MILAN, Italia**

KOCHA wa AC Milan, Stefano Pioli amewatia moyo wachezaji wake "kuota ndoto" ya kushinda taji la Ligi Kuu ya Italia, Scudetto, baada ya kuwa na mwanzo mzuri zaidi wa Serie A, shukrani kwa ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Atalanta, Jumapili.

Rossoneri walipata ushindi huo ugenini, dhidi ya Atalanta na walionekana kuwa bora zaidi na sasa wanashika nafasi ya pili, kwenye msimamo wakiwa na pointi 19 baada ya mechi saba.

Ushindi huo umewafanya kufikia rekodi ya kuanza msimu kwa ubora zaidi waliyoiweka msimu wa 2003-04, wakati walipolitwaa taji hilo.

Davide Calabria alianza kufunga sekunde ya 30 - likiwa bao la tatu la haraka zaidi kwenye Serie A kwa Milan tangu msimu wa 2004-05 la kwanza lilikuwa la Rafael Leao (sekunde sita dhidi ya Sassuolo) na Sulley Muntari (sekunde 18 dhidi ya Juventus).

Sandro Tonali na Leo kila mmoja alifunga bao moja na kuifanya Milan ikipaa na Pioli amekaribisha changamoto ya kuwania ubingwa.

"Tunatakiwa kucheza na kushinda kila mchezo, tulicheza kwa ubora sana na nguvu," alisema Pioli, wakati huu Milan ikitafuta bao lake la kwanza la Serie A tangu msimu wa 2010-11.

"Tonali anazungumzia kuhusu ubingwa wa Scudetto? Ni sawa vijana wanatakiwa kuota ndoto kuhusu hilo, kila mchezo tuna nafasi ya kuonyesha kwamba tunaweza kupambana.

"Ni safari ya miaka miwili, lakini sasa hatutakiwa kutosheka, lakini tunatakiwa kuwa wanyenyekevu na kuwaheshimu wapinzani wetu."

# HABARI MICHEZO

# 9,183,880

# JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 09/10/21 | 17:00 | Lugo vs Girona | 2.95 | 2.95 | 2.51 |
| 02. 09/10/21 | 17:00 | Hartlepool vs Northampton | 2.55 | 2.99 | 2.84 |
| 03. 09/10/21 | 17:00 | Bristol Rovers vs Carlisle | 2.55 | 3.09 | 2.75 |
| 04. 09/10/21 | 17:00 | Stevenage vs Exeter | 2.69 | 2.98 | 2.69 |
| 05. 09/10/21 | 17:00 | Sutton United vs Port Vale | 2.50 | 3.09 | 2.80 |
| 06. 09/10/21 | 17:00 | Barrow vs Leyton Orient | 2.55 | 3.14 | 2.70 |
| 07. 09/10/21 | 17:00 | Newport vs Bradford City | 2.79 | 3.19 | 2.45 |
| 08. 09/10/21 | 17:00 | Boreham Wood vs Dagenham and Redbridge | 2.49 | 3.22 | 2.68 |
| 09. 09/10/21 | 22:00 | Real Oviedo vs Sporting Gijon | 2.70 | 2.94 | 2.75 |
| 10. 10/10/21 | 08:00 | Matsumoto Yamaga vs Tochigi SC | 2.61 | 2.86 | 2.76 |
| 11. 10/10/21 | 15:00 | Real Sociedad B vs Ponferradina | 2.56 | 3.00 | 2.85 |
| 12. 10/10/21 | 19:15 | Alcorcon vs Burgos | 2.57 | 3.02 | 2.82 |
| 13. 10/10/21 | 22:00 | Fuenlabrada vs Leganes | 2.63 | 2.88 | 2.88 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMANNE - 05 - OKTOBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1553 | Muang Thong Utd vs Nong Bua Pitchaya | 1.64 | 3.95 | 5.00 |
| 14:00 | 4611 | BEC Tero Sasana vs Chonburi | 3.53 | 3.39 | 1.94 |
| 16:30 | 5167 | Catanzaro vs Fidelis Andria | 1.44 | 4.15 | 7.32 |
| 18:30 | 4390 | JJK Jyvaskyla vs OTP FC | 1.98 | 3.83 | 3.05 |
| 19:15 | 3653 | TPV Tampere vs EPS | 4.30 | 4.20 | 1.70 |
| 20:00 | 1118 | Viktoria Aschaffenburg vs FC Pipinsried | 2.24 | 3.52 | 2.75 |
| 20:00 | 3163 | Asker vs Kvik Halden | 1.87 | 3.88 | 3.30 |
| 20:00 | 3308 | Vasteras SK vs Gais | 1.99 | 3.56 | 3.61 |
| 20:00 | 5295 | Trelleborgs FF vs Landskrona Bois | 1.88 | 3.44 | 4.19 |
| 21:00 | 1563 | Argentino Rosario vs Centro Espanol | 2.47 | 2.81 | 3.00 |
| 21:00 | 1592 | Salford City vs Tranmere | 1.94 | 3.29 | 3.63 |
| 21:00 | 2010 | MK Dons vs Wycombe | 2.29 | 3.24 | 2.85 |
| 21:00 | 2265 | Yupanqui vs Deportivo Muniz | 3.24 | 2.80 | 2.33 |
| 21:00 | 2683 | Cheltenham vs Exeter | 1.78 | 3.55 | 3.99 |
| 21:00 | 2713 | Csyd Liniers vs Central Ballester | 1.84 | 3.10 | 4.36 |
| 21:00 | 2863 | CA Lugano vs Juventud Unida SM | 2.37 | 2.81 | 3.15 |
| 21:00 | 2949 | Sportivo Barracas vs Deportivo Paraguayo | 1.75 | 3.29 | 4.55 |
| 21:00 | 3331 | Crawley Town vs Leyton Orient | 2.41 | 3.29 | 2.66 |
| 21:00 | 3502 | Deportivo Merlo vs Los Andes | 3.05 | 2.66 | 2.56 |
| 21:00 | 3859 | Rotherham vs Scunthorpe | 1.36 | 4.54 | 7.14 |
| 21:00 | 3878 | Hartlepool vs Morecambe | 2.95 | 3.29 | 2.21 |
| 21:00 | 4120 | Defensores Cambaceres vs Puerto Nuevo | 2.28 | 2.95 | 3.14 |
| 21:00 | 4486 | Mansfield vs Sheffield Wed | 3.25 | 3.30 | 2.07 |
| 21:00 | 5269 | Gillingham vs Ipswich | 2.47 | 3.19 | 2.66 |
| 21:00 | 5422 | Crewe vs Wigan | 2.72 | 3.16 | 2.43 |
| 21:00 | 5955 | Charlton vs Southampton U21 | 1.46 | 4.45 | 5.41 |
| 21:10 | 5081 | Nueva Chicago vs Temperley | 2.69 | 2.69 | 2.84 |
| 21:45 | 1138 | Morpeth Town vs Radcliffe Borough | 2.47 | 3.34 | 2.56 |
| 21:45 | 1394 | Oxford Utd vs Stevenage | 1.36 | 4.63 | 6.95 |
| 21:45 | 1505 | Nantwich Town vs Gainsborough | 2.54 | 3.27 | 2.54 |
| 21:45 | 1549 | Enfield Town vs Kingstonian | 2.43 | 3.40 | 2.57 |
| 21:45 | 1724 | Woking vs Dagenham and Redbridge | 3.02 | 3.51 | 2.13 |
| 21:45 | 1858 | Barrow vs Fleetwood Town | 2.86 | 3.25 | 2.28 |
| 21:45 | 2309 | Basford United vs Utd of Manchester | 2.30 | 3.55 | 2.90 |
| 21:45 | 2320 | Wealdstone vs Solihull Moors | 3.52 | 3.33 | 2.00 |
| 21:45 | 2381 | Altrincham vs Grimsby | 3.07 | 3.32 | 2.18 |
| 21:45 | 2392 | Stalybridge vs Grantham Town | 1.88 | 3.48 | 3.63 |
| 21:45 | 2432 | Bamber Bridge vs South Shields | 3.05 | 3.55 | 2.22 |
| 21:45 | 2672 | Witton Albion vs Hyde United FC | 2.47 | 3.49 | 2.47 |
| 21:45 | 2907 | Kings Lynn vs Barnet | 2.07 | 3.48 | 3.19 |
| 21:45 | 3242 | Lancaster City vs Stafford Rangers | 2.18 | 3.35 | 2.96 |
| 21:45 | 3351 | Dover vs Aldershot | 2.60 | 3.53 | 2.40 |
| 21:45 | 3496 | Accrington vs Leicester City U21 | 1.64 | 3.97 | 4.26 |
| 21:45 | 4258 | Bromley vs Weymouth | 1.56 | 4.19 | 4.87 |
| 21:45 | 4499 | Yeovil vs Maidenhead U | 2.11 | 3.56 | 3.03 |
| 21:45 | 4537 | Boreham Wood vs Torquay | 2.14 | 3.42 | 3.08 |
| 21:45 | 4583 | Southend vs Eastleigh | 2.02 | 3.57 | 3.22 |
| 21:45 | 4907 | Wrexham vs Chesterfield | 1.83 | 3.53 | 3.92 |
| 21:45 | 5348 | Buxton FC vs Whitby Town | 2.29 | 3.19 | 2.90 |
| 21:45 | 5856 | Halifax vs Notts County | 2.98 | 3.47 | 2.17 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



# ANCELOTTI ARIDHIKA KIPIGO REAL MADRID

**MILAN, Italia**

CARLO Ancelotti amesema kiwango kilichoonyeshwa na Real Madrid katika kipigo cha mabao 2-1 kutoka kwa Espanyol, kilikuwa kibovu zaidi tangu aliporudi klabuni hapo.

Iliendelea kuwa wiki mbaya kwa 'Los Blancos' hao wakati walipopoteza kwenye mchezo huo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, pale kwenye Uwanja wa RCDE, Jumapili.


Katikati ya wiki, Real Madrid pia ilichezea kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa timu ya nchini Moldavia, Sheriff, kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na juzi wakachapwa kwa mabao ya Raul de Tomas na Aleix Vidal.

Karim Benzema alifunga bao la kufutia machozi, lakini Ancelotti alishuhudia kikosi chake kikipoteza pointi tatu kabla ya ligi hiyo, kusimama kwa ajili ya kupisha mechi za kimataifa.

Raia huyo wa Italia alisema baada ya mchezo huo akiwaambia waandishi wa habari: "Ulikuwa mchezo mbovu zaidi kwa msimu huu hadi sasa."

"Tulicheza vibaya, hakuna cha kusema zaidi. Tunatakiwa kubadilisha mtazamo na akili yetu, ilikuwa ni wiki mbaya sana kwetu.

"Kufungwa huku halikuwa tukio la bahati mbaya kwani tulistahili kupoteza mchezo. Tunahofu kwa sababu tumepoteza mechi mbili mfululizo na huu si utamaduni wa klabu hii, tunatakiwa kurekebisha makosa yetu."



# Conte: Chelsea haijui kumtumia Lukaku

**LONDON, England**

KOCHA wa zamani wa Inter Milan, Antonio Conte, amesema klabu ya Chelsea imeshindwa kutambua jinsi gani wanaweza kumtumia mshambuliaji wao, Romelu Lukaku.

Lukaku alikuwa akifanya kazi na Conte baada ya kumsajili mshambuliaji huyo, kule Inter Milan akitokea Manchester United mwaka 2019.

Lukaku alirejea Stamford Bridge kwa kipindi cha pili katika dirisha la usajili la Januari kwa kitita cha pauni milioni 98.

"Nadhani ana uwezo wa kufanya vizuri zaidi, ukiacha vyote mbinu zake. Yupo katika ubora mkubwa sana, lakini mchezaji anapaswa kuboresha kiwango chake mpaka pale atakapostaafu," alisema Conte aliiambia Sky Sport Italia.

"Wakati wa mchezo, kuna muda Lukaku anapaswa kurudishwa mchezoni, lakini zaidi ya hivyo ni mmoja kati ya mshambuliaji hatari kucheza dhidi yake, kwa sababu anaweza kufanya hatari eneo lolote katika uwanja.

"Ukiwa na mshambuliaji kama yule, unahitaji kumtumia na sidhani kama Chelsea wameweza kutambua njia ya kumtumia mpaka sasa." aliongeza Conte.

Michezo
Jumanne Oktoba 5, 2021
Nipashe



Guardiola ashangaa Milner kutolambwa kadi nyekundu

UKURASA 21

# SIMBA YASHTUA KUFUZU KOMBE LA DUNIA 2022

●●●Nusu ya wachezaji wake waitwa kuchezea timu zao za taifa, Gomes atoa neno...

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Bara, wamedhihirisha timu yao kuundwa na wachezaji wa kiwango cha juu zaidi ya klabu zote Afrika Mashariki na Kati baada ya nyota wao 16 kati ya 32 waliosajiliwa na timu hiyo kuitwa kwenda kuzitumikia timu zao za taifa kuwania kufuzu Kombe la Dunia nchini Qatar 2022, imefahamika.

Simba ambayo Jumapili ijayo ya Oktoba 17, itashuka katika Uwanja wa Stade National nchini Botswana kuwavaa wenyeji wao, Jwaneng Galaxy FC kwenye mechi ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika, tayari imewaruhusu nyota wake wote 16 walioitwa na timu zao kwenda kuzitumikia kuelekea michezo miwili nyumbani na ugenini itakayopigwa Oktoba 7 na 10, mwaka huu.

Hata hivyo, Simba ingeweza kutoa wachezaji 17, lakini Kocha Mkuu wa timu ya Taifa ya Tanzania 'Taifa Stars, Kim Poulsen, alilazimika kumwengua katika kikosi chake beki wa kulia Shomari Kapombe kutokana na majeraha aliyoyapata wakati akiitumikia timu yake dhidi ya Dodoma Jiji FC wiki iliyopita.

Wachezaji walioitwa wa Simba kwa upande wa Taifa Stars ni tisa, ambao ni Aishi Manula, Israel Patrick Mwenda, Mohamed Hussein, Kennedy Juma, Jonas Mkude, Erasto Nyoni, Mzamiru Yassin, John Bocco na Kibu Denis.

Kwa upande wa nyota wa kimataifa ni wachezaji saba; Peter Banda na Duncan Nyoni (Malawi), Rally Bwalya (Zambia), Taddeo Lwanga (Uganda), Meddie Kagere (Rwanda), Joash Onyango (Kenya) na Henock Inonga Baka (DR Congo).

Akizungumzia maandalizi ya mechi hiyo yao ijayo dhidi ya Jwaneng Galaxy FC, Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, alisema pamoja na kuondoka kwa idadi kubwa ya wachezaji kwenda kujiunga na timu zao za taifa, nyota wake ambao hawakuitwa wataendelea na mazoezi hadi wenzao watakaporejea.

"Tuliwapa wachezaji mapumziko baada ya mechi ngumu dhidi ya Dodoma Jiji na leo [jana], tutaanza mazoezi tukiwa na wachezaji ambao hawakuitwa na timu zao za taifa kwa ajili ya mechi za kuwania kufuzu Kombe la Dunia na kuendelea hadi hapo wengine watakaporejea kujiunga na wenzao," alisema.

Aidha, Gomes alisema kurejea kwa kiungo mshambuliaji wake, Bernard Morrison kuelekea mchezo huo wa Ligi ya Mabingwa Afrika kunaongeza matumaini makubwa ya kufanya vizuri.

"Michezo mitatu iliyopita imekuwa ya faida kubwa kwetu kutuandaa na mashindano mbalimbali tutakayoshiriki mwaka huu, kwa namna ninavyokiona kikosi changu nashawishika kusema tupo tayari.

"Tuna mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika, michuano ambayo ni muhimu kwetu, lazima tujiandae kufanya vizuri katika hatua hii na ni jambo zuri kuona tuna nafasi ya kumtumia tena Bernard Morrison katika mashindano hayo," alisema.

Morrison alikuwa nje akitumikia adhabu ya kufungiwa mechi tatu kutokana na kuonyesha vitendo vya utovu wa nidhamu kwenye mechi ya fainali ya Kombe la FA dhidi ya Yanga ambayo ilipigwa Uwanja wa Lake Tanganyika na mabingwa hao wa Ligi Kuu Bara kushinda 1-0, bao lililofungwa na Taddeo Lwanga.

Hata hivyo, sasa Morrison amemaliza adhabu hiyo baada ya kukosa mechi ya Ngao ya Jamii dhidi ya Yanga na michezo miwili ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Biashara United na Dodoma Jiji FC, ambayo mmoja Simba ilitoka suluhu na kushinda bao 1-0.




Duncan Nyoni, 'chuma hiki cha reli' Simba kimeitwa Taifa Malawi

## Kibu fasta ajiunga Stars kuivaa Benin

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Simba, Kibu Denis ameingia kambini kujiunga na kikosi cha timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), kinachojiandaa na mechi ya kuwania kufuzu Kombe la Dunia Qatar 2022 dhidi ya Benin.

Awali, licha ya Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Kim Poulsen kueleza mchezaji huyo kuwa katika mipango yake kuelekea mchezo huo, hakujumuishwa katika kikosi chake cha wachezaji 23 alichokiita kutokana na suala la utata wa uraia wake.

Lakini mwishoni mwa wiki taarifa iliyotolewa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ilieleza: "Kufuatia mamlaka aliyopewa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, kwa mujibu wa Sheria ya Uraia, Sura ya 357 (Rejeo la 2002), baada ya kupokea ombi lililoletwa kwake na TFF, amempa uraia wa Tanzania Mchezaji wa Mpira wa Miguu, Kibu Denis Prosper, Sept. 30".

Na baada ya taarifa hiyo Kibu hakutaka kulaza damu katika kulipambania taifa kwani 'fasta' alijiunga na wenzake kikosini kujiandaa na mechi hiyo itakayopigwa keshokutwa, Alhamisi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kabla ya kurudiana nchini Benin Jumapili wiki hii.

Kuelekea mchezo huo, Ofisa Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Cliford Ndimbo, alisema tayari kikosi hicho kimeingia kambini na kuendelea na mazoezi kwa ajili ya mchezo huo.

"Kwa upande wa uongozi kila kitu kinaenda vizuri kutekeleza yale anayohitaji kocha Poulsen na sasa kazi kubwa imebaki kwake kuhakikisha anafanya majukumu ili kufikia malengo yanayotarajiwa na Watanzania".

Kwa upande wa Kocha Poulsen alisema ana imani mechi dhidi ya Benin itakuwa ya ushindani mkubwa kutokana na ubora wa wapinzani wao hao hasa kutokana na muda mchache wa kujiandaa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >